SUPA JACKPOT
TZS. 1,154,861,566
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

Jumamosi Septemba 23, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581442
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**Marekani** yatangaza ufadhili mpya kwa Tanzania UKURASA 3



**Watoto** UKURASA 17 wapelekwa hospitalini madai kula keki zenye bangi



**Serikali** UK. 10 Zanzibar yatoa kauli kuhusu uwekezaji Bandari



# Upigaji wa mamilioni ya fedha watikisa

• **WAZIRI** Mkuu anusa ufisadi mwingine Kigoma, atuma timu, DED asimamishwa utendaji usioridhisha... *Ukurasa 2 & 3*




UKURASA 11

## Walimu, wanafunzi sekondari mbaroni tuhuma kuwafanyia mitihani ya darasa la 7

UKURASA 2



Baadhi ya wafugaji wakiangalia moja ya ng'ombe waliojeruhiwa kwa risasi baada ya kutokea kwa mgogoro kati yao na wakulima katika Kijiji cha Lembapuli, Kiteto mkoani Manyara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mgogoro wakulima, wafugaji wageuka uwanja wa mauaji

UKURASA 8

**MICHEZO** **RASMI INONGA KUIKOSA DYNAMOS** UK.24

**MAONI** UK.6

# Upigaji mamilioni ya fedha watisha

**Na Mwandishi Wetu**

NI upigaji wa mamilioni ya fedha za maendeleo zinazopelekwa katika mamlaka za serikali za mitaa.

Hivyo ndivyo inavyoweza kuelezwa baada ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kuibua ufisadi mpya wa mamilioni katika wilaya ya Kigoma na kuahidi kupeleka timu maalum ili kuchunguza fedha zinazopotea kinyemela kupitia mtandao wa watumishi wasio waaminifu. Majaliwa aliahidi hilo jana wakati akizungumza na viongozi wa dini, serikali, Chama Cha Mapinduzi (CCM) na watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kwenye ukumbi wa NSSF, Kigoma mjini.

"Hapa Manispaa mnapokea fedha, zinakaa kwenye akaunti kwa muda halafu zinapotea, hazijulikani zimefanya nini? Nitaleta timu waje wafuatilie hapa Kigoma, waende hadi TAMISEMI (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) ili tuone huo mnyororo unakwenda wapi," alisema.

Waziri Mkuu alisema fedha zinazotoka serikali kuu huwa zinatumwa na maelekezo mahsusi ya kwamba, zinakwenda kufanya shughuli gani na za makusanyo ya ndani uamuzi wa matumizi yake ni lazima yafanywe na baraza lote la madiwani. Majaliwa alitoa mfano wa Manispaa ya Kigoma kuwa ilipokea Sh. milioni 500 kutoka Ofisi ya Rais-TAMISEMI ambazo zilikaa kwenye akaunti kwa muda mrefu na baadaye zikatoweka na hazijulikani zilitumika kwa kazi gani. "Kuna kiasi kingine cha Sh. milioni 447 kilitumwa Kigoma. Wakati zinaandaliwa kutoka mkurugenzi akazuia. Hongera mkurugenzi na uendelee kuzuia. Sisi tunamfuatilia mkurugenzi aliyekuwapo kwa sababu anajua zile Sh. milioni 500 zilitokaje," alisema.

Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, Waziri Mkuu alisema wanakabiliwa na matatizo mengi yakiwamo matumizi mabaya ya fedha, makusanyo kidogo sababu ya malumbano, mawakala kukaa na fedha mikononi badala ya kuzipeleka benki, Baraza la Madiwani kukosa taarifa za fedha na kutumia fedha za miradi kulipana posho.

"Kuna watu wamejilipa Sh. milioni 11 zikiwa ni posho ya safari ya Dodoma. Pia wametumia Sh. milioni sita kufanya service (matengenezo) ya gari, hili ni gari la aina gani? Wengine wametumia Sh. milioni tisa kwenye sherehe za Siku ya Mtoto wa Afrika na wengine wamejilipa Sh. milioni 14. 8 kwenda kwenye sherehe za Nanenane Tabora, hivi mlikaa siku ngapi huko?" alihoji.

Waziri Mkuu alisema kuna tume ya TAMISEMI ilikwenda kufanya uchunguzi kwenye halmashauri hiyo kuhusiana na matatizo hayo na ameitaka ikamilishe kazi yake haraka na kuiwasilisha kwa Waziri wa Nchi, OR-TAMISEMI.

"Tume ikamilishe kazi haraka, akabidhiwe Waziri. Ninamwagiza Mheshimiwa Waziri Mchengerwa akipokea taarifa ya tume hiyo, aje Kigoma achukue hatua," aliagiza.

Waziri Mkuu alitumia fursa hiyo kuwaasa watumishi wa Halmashauri zote mbili waache makundi kwani yanasababisha migongano na kuzorotesha utoaji huduma kwa wananchi.

"Migogoro yenu inasababisha upotevu wa rasilimali watu na fedha," alisema.

Waziri Mkuu amemaliza ziara yake ya siku tatu mkoani Kigoma na ameanza ziara ya siku tatu mkoani Kagera.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na watumishi Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Mjini na Kigoma Vijijini, mkoani Kigoma jana. **PICHA: OWM**

# TIC yawatoa hofu wawekezaji kukatika umeme

**Na Halfani Chusi**

MWENYEKITI wa Bodi ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Dk. Binilith Mahenge, amewatoa hofu wawekezaji kuhusu kukatika kwa umeme na kusababisha hasara kuwa suala hilo linashughulikiwa.

Dk. Mahenge aliyasema hayo jana Dar es Salaam, alipofanya ziara katika viwanda vinavyomilikiwa na wawekezaji wa ndani kwa lengo la kusikiliza kero zinazowakabili na kutafuta namna ya kuzitatua.

Akiwa katika kiwanda kinachotengeneza bidhaa za plastiki cha PLASCO kilichoko Chang'ombe, alisema kazi kubwa ya kituo hicho ni kuvuta wawekezaji wa ndani na nje ya nchi pamoja na kuishauri serikali namna bora ya kuimarisha sekta hiyo.

Watanzania wengi, alisema wana uwezo wa kuwekeza kama ilivyo kwa wageni na kwamba wanapaswa kutumia fursa waliyo nayo ili kuongeza ajira kwa wananchi.

"Watanzania wanatakiwa kujua fursa za uwekezaji ni kwa wote. Serikali inavutiwa zaidi na wawekezaji wa ndani kwa sababu wao ndio wana uwezo wa kuajiri Watanznaia wengi na ujuzi ukabaki ndani ya taifa letu.

"Nimepokea changamoto kwa PLASCO ya kukatika kwa umeme na baadhi ya viwanda kukumbwa na mafuriko kipindi cha mvua. Tunakwenda kuzifanyia kazi lakini hili suala la umeme ninaamini utakapokamilika mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere itakuwa suluhu yake," alisema.

Dk. Mahenge alitaja faida za kuwapo kwa viwanda vingi ndani ya nchi kuwa ni pamoja na kupungua kwa gharama ya bidhaa na kupatikana kwa wakati pamoja na kuongeza ajira na kukuza uchumi.

"Zamani ili usajili kampuni, ilikuwa lazima uende Wakala wa Usajili Biashara na Leseni (BRELA), uwe na vibali vya kufanya kazi ndani ya nchi, ufuate taratibu za Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)," alisema. Lakini kwa sasa, alisema imetungwa sheria mpya ya uwekezaji ambayo moja ya jukumu lake ni kuhakikisha vitengo vyote vya serikali kuhusu uwekezaji vinazungumza lugha moja.

Alisema hivi karibuni watazindua mfumo ambao mwekezaji anaweza akafanya kila kitu kwa kutumia mtandao ikiwamo kujisajili kokote aliko.

Mkurugenzi Mtendaji wa PLASCO, Alighulam Hussein, aliishukuru serikali kwa kuwatembelea akisifu ziara hiyo kwao imekuwa tiba kwenye mambo mengi.

Alisema kutokana na mazingira mazuri ya uwekezaji, wanajenga kiwanda kingine Kigamboni ambacho kitakuwa kikubwa zaidi kwa kuwa eneo walilopo kwa sasa ni dogo.

## Walimu, wanafunzi wa sekondari mbaroni tuhuma kuwafanyia mitihani darasa saba

**Na Elizabeth Selemani,** SENGEREMA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza linawashikilia watu saba ambao ni wasimamizi wa mitihani pamoja na wanafunzi wa sekondari wanaotuhumiwa kufanya mitihani ya kumaliza darasa la saba iliyofanyika hivi karibuni.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilbroad Mutafungwa, alisema katika taarifa yake jana kuwa watuhumiwa hao ni kutoka katika Shule ya Msingi Igulumuki na Shule ya Sekondari Sima zilizoko wilayani Sengerema.

Mutafungwa alisema waliokamatwa kwa tuhuma hizo ni Msimamizi Mkuu wa Mtihani Shule ya Msingi Igulumuki, Machael Sheusi (35) ambaye ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Sima.

Alisema tukio hilo lilitokea Septemba 13, mwaka huu, saa 8:00 mchana katika Shule ya Msingi Igulumuki, wakati kamati ya mitihani ya wilaya ya Sengerema ilipotembelea shuleni hapo kwa ajili ukaguzi na kubaini kufanyika kwa udanganyifu huo.

Mutafungwa aliwataja watuhumiwa wengine kuwa ni Musa Mwashihava (38), mwalimu wa Shule ya Sekondari Kilabela ambaye ni msimamizi wa mtihani mkondo namba mbili na tatu, Bonasi Balozi (33) mwalimu wa Shule ya Sekondari Buzilasoga ambaye alikuwa msimamizi wa mtihani mkondo namba tatu na Azizi Mohamed (36), Mwalimu wa Taaluma, Shule ya Msingi Igulumuki.

Pia alisema wamewakamata wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Sima wanaodaiwa kuhusika katika udanganyifu huo ambao ni Shadrack Bwana (14), Revocatus Paulo (14) na Pendo Bukoma (14), wote wakazi wa Igulumuki.

Mutafungwa alisema Jeshi la Polisi linaendelea kumsaka mtuhumiwa anayedaiwa kuhusika na udanganyifu huo ambaye ni Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Igulumuki, Amlesian Mufungo, aliyetokomea kusikojulikana. Alisema watuhumiwa hao wameshahojiwa kwa tuhuma za kuwachukua wanafunzi wa sekondari ili kuwafanyisha mitihani hiyo kwa niaba ya wanafunzi wa darasa la saba.

"Watuhumiwa wote wamehojiwa kwa kina na watafikishwa mahakamani haraka iwezekanavyo baada ya upelelezi kukamilika," alisema.

Hivi karibu, baada ya Nipashe kupata taarifa ya udanganyifu huo, ilimtafuta kwa njia ya simu Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mwanza, Martin Nkwabi, ambaye alithibitisha kuwapo kwa suala hilo na kueleza kuwa hatua zingine zitafanywa na Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA).

"Sina mamlaka ya kulitolea ufafanuzi tukio hilo, lakini taratibu zote zitafanyika chini ya baraza la mitihani Taifa," alisema Nkwabi.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme (katikati) akishiriki ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Nyahanga, Manispaa ya Kahama juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Marekani yatangaza ufadhili mpya Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, na Kiongozi Mkuu wa USAID Power, Samantha Power, wameangazia maendeleo ya demokrasia Tanzania na kutangaza ufadhili mpya kutoka serikali ya Marekani na wahisani wengine nchini humo.

Ufadhili huo mpya umetangazwa katika Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa ambao utasaidia juhudi za maendeleo ya serikali na kuwezesha uboreshaji wa huduma za umma kama sehemu ya Mpango wa USAID wa 'Democracy Delivers'.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ubalozi wa Marekani nchini, katika hafla ya Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) 'Democracy Delivers' kando ya Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa jana, viongozi hao walihimiza wahisani na washirika wa sekta binafsi kuwekeza Tanzania.

Taarifa hiyo ilisema Waziri Blinken na Kiongozi Mkuu wa Shirika la USAID Power, kwa ushirikiano na Ford Foundation na Rockefeller Foundation, walihimiza hilo kwa Tanzania na kwa nchi zingine zinazopiga hatua za kidemokrasia.

Taarifa hiyo ilisema Balozi wa Tanzania nchini Marekani, Elsie Kanza, alijumuika na viongozi kutoka kundi la kwanza la nchi zitakazofaidika na ufadhili kutoka Mpango wa USAID wa Democracy Delivers. Ilizitaja nchi hizo ni pamoja na Armenia, Jamhuri ya Dominica, Ecuador, Malawi, Maldives, Moldova, Nepal, Tanzania na Zambia.

Ilisema kuwa, nchi hizo zimejadili njia za kuelekeza rasilimali mpya ambazo zitasaidia wana mageuzi na wananchi katika nchi zao ambao wanajenga demokrasia yenye manufaa kwa wote.

"Mpango wa USAID wa Democracy Delivers uliozinduliwa mwaka 2022 na Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Blinken na Kiongozi Mkuu wa USAID Power, unalenga kuongeza msaada, rasilimali na umuhimu katika nchi zinazopitia kipindi cha fursa za kidemokrasia," ilisema taarifa hiyo.

Mkurugenzi Mkazi wa USAID Tanzania, Craig Hart, alisema: "Uhusiano kati ya watu wa Marekani na Watanzania ambao umeendelea kuwa imara kwa zaidi ya miaka 60, unatokana na maadili na matarajio ya pamoja. Lengo ni moja: Tanzania yenye amani na ustawi, ambapo wananchi wote wanaweza kutambua uwezo wao kamili na kutumia uhuru wao wa kimsingi."

Hart aliipongeza Tanzania na viongozi wake kwa kuanza kufanya mageuzi muhimu ya kidemokrasia yanayowapa fursa wananchi kupaza sauti.

Pia kitendo cha kupanua nafasi ya kiraia na uhuru wa vyombo vya habari na kushirikiana tena na jumuiya ya kimataifa. Alisema maboresho hayo tayari yameanza kuboresha maisha ya Watanzania.

Katika hafla ya Mpango wa USAID Democracy Delivers kwenye Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Marekani ilitangaza ahadi za kuisaidia Tanzania.

USAID inashirikiana na Bunge la Marekani kutoa hadi Dola milioni tano ili kuunga mkono juhudi za Wizara ya Fedha ya Tanzania kuandaa, kutekeleza, na kudumisha mfumo wa ununuzi wa umma wa kidijitali unaozingatia uundaji wa tovuti ya ununuzi wa kidijitali. Tovuti hii itaongeza uwazi na ufanisi wa manunuzi huku ikipunguza fursa za ufisadi.

# DED mwingine asimamishwa kazi

**Na Vitus Audax**

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega mkoani Simiyu, Veronica Sayore, amesimamishwa kazi kupisha uchunguzi kwa kile kinachoelezwa kuwa utendaji usioridhisha.

Hatua hiyo imechukuliwa zikiwa zimepita saa kadhaa baada ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, Kigoma, Zainab Mbunda, na Mweka Hazina wa halmashauri hiyo, Majjid Mabanga, kusimamishwa kazi na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipokuwa ziarani.

Katika taarifa iliyotolewa jana, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amemsimamisha kazi Sayore kupisha uchunguzi.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, hatua hiyo imefikiwa kutokana na Waziri Mchengerwa kupokea taarifa na malalamiko kuhusu utendaji kazi usioridhisha wa mkurugenzi huyo na kwamba hana ushirikiano kwa viongozi wenzake.

Taarifa hiyo pia ilisema mkurugenzi huyo amekuwa akishindwa kuwashirikisha viongozi na watendaji wenzake katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Waziri Mchengerwa amemwagiza katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI kuunda timu ya uchunguzi dhidi ya mwenendo wa utendaji kazi mkurugenzi huyo pamoja na matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Busega.

Kadhalika, Mchengerwa amewataka wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa kusimamia dhana ya ushirikishwaji wa viongozi, watendaji na wananchi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mchengerwa amewaagiza kuweka uhusiano mzuri baina yao viongozi na watendaji ili kuhakikisha wanajenga timu yenye umoja katika utekelezaji wa jukumu la kuwahudumia wananchi.

Kusimamishwa kwa Mkurugenzi Sayore ni mwendelezo wa uwajibikaji baada ya juzi Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwa mkoani Kigoma, kumsimamisha Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza na Mweka Hazina wake, baada ya kutokuridhishwa utekelezaji wa ujenzi wa hospitali.

# Elimu matumizi bora nishati kutolewa

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) linashirikiana na serikali katika utekelezaji wa mradi wa matumizi bora ya nishati kwa lengo la kupunguza gharama kubwa za malipo.

Mradi huo wa miaka mitatu unafadhiliwa na UNDP na Umoja wa Ulaya (EU) ambazo zimetoa Euro milioni tisa (zaidi ya Sh. bilioni 23.9) na umeanza kwa kutoa elimu kwa watumiaji wakubwa wa nishati kama viwanda na majengo makubwa ya biashara.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii jana mkoani Dar es Salaam, Mtaalamu Mshauri wa Masuala ya Matumizi Bora ya Nishati kutoka UNDP, Robert Washija, alisema mradi huo una maeneo saba ya utekelezaji ikiwamo kutengeneza mpango mkakati wa taifa wa matumizi bora ya nishati ambao utaweka utaratibu maalumu wa matumizi. Washaija alisema eneo la pili ni kuweka utaratibu wa kuwa na vifaa bora vinavyoingia nchini ambavyo vinatumia umeme mdogo, na kutengeneza kanuni na taratibu ambazo zitatoa muongozo wa namna majengo yatakavyokuwa yanajengwa.

"Jengo ukiliweka katika utaratibu mzuri linapunguza hata matumizi ya umeme, eneo la nne ni kuwa na 'data energy' katika taifa kwa sababu kwa sasa ukiangalia kuna shida kubwa ya kupata takwimu kila taasisi wana taarifa zao, kwa hiyo tunataka kuziweka kwa pamoja.

"Eneo la tano ni kufanya ukaguzi wa matumizi ya nishati, tunataka kuonyesha Watanzania kwamba, nishati inaweza ikafanyiwa ukaguzi ukajua ni wapi unatumia vibaya ili uangalie namna ya kuweka vitu vizuri katika jengo lako na ikakupunguzia gharama kubwa za umeme," alisema Washija.

Eneo la sita alilitaja ni kukuza uwezo na ujuzi kwa wataalamu na wananchi kwa ujumla, kuhusu usimamizi na ukaguzi wa nishati na wamekiongezea uwezo Chuo cha Teknolojia (DIT) kwa kununua vifaa vya ufundishaji katika maabara zao.

Alitaja eneo linguine, alisema ni kujenga uwezo kwa wananchi ambapo kwa mwaka huu wametangaza nafasi 10 za ufadhili wa masomo ambazo zitatolewa kwa wanawake watakaosoma shahada ya uzamili chuoni hapo.

Meneja Usimamizi wa Vifaa katika jengo la kibiashara la PSSSF, Hemed Mndeme, alisema moja ya maeneo ambayo yanaongeza gharama ya uendeshaji ni ya umeme, akibainisha unachangia zaidi ya asilimia 60 ya matumizi kwa mwezi.

## WANATAFUTWA NA POLISI TUHUMA ZA WIZI ARS/ RB: 8837/2023



**JINA : MOSES ALFRED MABULA**
**KABILA : MSUKUMA WA MWANZA. MAKAZI : DARAJA MBILI ARUSHA UMRI MIAKA :46**




**JINA : LAZARO RICHARD PYUZA**
**KABILA : MNYIRAMBA**
**MZALIWA WA MKOA WA SINGIDA MKAZI WA DARAJA MBILI ARUSHA UMRI MIAKA 37**

217604702

Watuhumiwa wa uwizi katika kampuni ya **Predators Safari Club Ltd** iliyopo Arusha maeneo ya Sakina.

***Yeyote atakayefanikisha kutoa taarifa za kukamatwa kwa watuhumiwa hawa zawadi itatolewa ya Tsh:2,000,000/=( milion mbili)***

**Kwa mawasiliano piga simu namba 0767 445344 / 0716 082447 ama toa taarifa kituo cha Polisi.**




Mkuu wa Wilaya ya Kahama, mkoani Shinyanga, Mboni Mhita (kushoto), akipokea kipeperushi chenye ujumbe wa kampeni ya Tuwajibike chenye kauli mbiu ya "Risiti yako Maendeleo yako" kutoka kwa Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA ) mkoa wa kikodi Kahama, Wisaka Kamwamu wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Mahakama yasema kifo aliyefia polisi kilitokana na kujinyonga

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kivukoni, Kinondoni, Dar es Salaam imesema imeridhika kuwa kifo cha Stella Moses kilitokana na kujinyonga akiwa mahabusu ya Kituo cha Polisi Mburahati alikokwenda kujisalimisha.

Stella alifariki dunia usiku wa Desemba 20, 2020 akiwa katika mahabusu ya Kituo hicho na wanafamilia hawakukubaliana na maelezo hayo badala yake wakaomba ufanyike uchunguzi huru kujiridhisha chanzo cha kifo chake.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Hakimu Mkazi Jackline Rugemalira, chini ya Mahakama ya Korona, baada ya mleta maombi kuiomba mahakama iridhie kufanya uchunguzi wa kifo cha utata cha Stella akiwa chini ya mahabusu ya polisi.

Alisema mahakama imeangalia mamlaka yake hasa suala la muda kuwa ni muda ambao Korona anatakiwa kuendesha uchunguzi wa kifo cha utata, lakini akasema katika Sheria ya Uchunguzi wa Vifo Vyenye utata, hakuna kifungu maalum ambacho kinatamka kufanya uchunguzi huo.

"Sheria ya ukomo wa muda inatoa nafasi ya kufunguliwa shauri la uchunguzi ndani ya siku 60, lakini tayari mahakama ilishaanza kusikiliza ushahidi ikaona inatakiwa kuendelea kusikiliza ushahidi huo.

"Kwa mazingira ya shauri hili mleta maombi alitakiwa kuleta maombi mapema ipasavyo baada ya kupata taarifa za kifo ili shauri liendelee kwa sababu hayo yote hayakufanyika, mahakama inaona utaratibu wa kuleta maombi haukuwa sahihi," alisema.

Hakimu Rugemalira alisema kuhusu ushahidi ni wajibu wa Mahakama ya Korona kuonyesha marehemu ni nani na kifo chake kilisababishwa na nini.

" Hakuna ubishi kuwa marehemu anaitwa Stella Moses ambaye alikutwa amening'inia kwenye mahabusu ya polisi," alisema Hakimu Rugemalira

Pia alisema mahakama inazingatia ushahidi ambao ni taarifa ya uchunguzi wa mwili wake ya Februari 25, 2020 inayoonyesha kuwa kifo hicho kimesababishwa na jeraha kichwani na kufeli mfumo wa kupumua.

"Shahidi mtaalamu aliyechunguza mwili huo alisema mfupa wa shingo ulikuwa umevunjika na jeraha kichwani kwake lakini haikuelezwa lilisababishwa na nini," alisema na kuongeza kuwa shahidi huyo alidai kuwa pamoja na kwamba sababu za kifo ni jeraha kichwani na kushindwa kupumua, kinachoanza ni kukosa hewa na jeraha linaweza kufuata.

"Kwa ushahidi wa ripoti ya daktari kuwa marehemu alikutwa na mauti kwa jeraha kichwani na kwa sababu shahidi waliomfikisha hapo hospitalini walieleza kuwa marehemu alifika kituoni hapo kutokana na tuhuma zilizokuwa zinamkabili Tunduma,

pia alikuwa na askari ambaye alielekeza amweke mahabusu, ndipo jioni walipokuta mwili wake unaning'nia kwenye mlango wa choo cha wanawake," alisema.

Hakimu Rugemalira alisema kutokana na ripoti ya daktari, kilichosababisha kifo ni kufeli kupumua na jeraha lakini hakuna shahidi mwingine aliyeeleza kuwa jeraha lilitokana na nini, kwa hiyo mahakama inaridhika kifo kilitokana na yeye mwenyewe kujinyonga.

Katika shauri hilo, mleta maombi aliwakilishwa na Peter Madeleka na Jamila Ilomo na upande wa wajibu maombi uliwakilishwa na Wakili wa Serikali, Job Mrema

Wajibu maombi ambao ni Mkuu wa Jeshi la Polisi na wenzake waliiomba mahakama isifanye uchunguzi huo hadi pale maombi waliyoyawasilisha yatakaposikilizwa na kutolewa uamuzi.

Baada ya mahakama kusikiliza hoja za pande zote, ilikubaliana na hoja za upande wa Jamhuri na kuanza kusikiliza shauri hilo kwa kumwita kutoa ushahidi aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, Ramadhani Kingai na aliyekuwa Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa.

Shauri hilo lilifunguliwa na shemeji wa marehemu, Emmanuel Kagongo, kwa niaba ya familia dhidi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam (ZPC) na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni (RPC), Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kipolisi Mburahati (OCD), Mkurugenzi Mtendaji Hospitali ya Taifa Muhimbili na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Katika hati ya maombi hayo ya jinai mchanganyiko namba 3 ya mwaka 2022, mleta maombi aliomba mahakama iridhie kufanya uchunguzi huru ili kujua ukweli wa mazingira ya kifo cha ndugu yao.

# Silaa ataka watumishi ardhi kukaa 'mguu sawa' mabadiliko

**Na Munir Shemweta**

WAZRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, amewataka watumishi wa ardhi nchini kuwa tayari kwa mabadiliko yenye lengo la kuiboresha sekta hiyo.

Silaa aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na watumishi wa sekta ya ardhi katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ikiwa ni mara yake ya kwanza kukutana nao tangu ateuliwe kuwa waziri wa wizara hiyo.

"Tuna kazi kubwa ya kufanya reforms (mabadiliko) nyingi katika wizara hii ambazo zinalenga kumhudumia Mtanzania. Mifumo ya TEHAMA (teknolojia ya habari na mawasiliano) katika upimaji wetu, nchi inatakiwa kupimwa na kupangwa ili kupunguza migogoro ya ardhi," alisema Silaa. Aliwaambia watumishi wa sekta ya ardhi kutambua kuwa waziri aliyekuja anafanya kazi kubwa ya kumsaidia Rais katika sekta ya ardhi, hivyo ni lazima kufanyike mabadiliko makubwa.

Kwa mujibu wa Waziri Silaa, mabadiliko yanayofanyika yanalenga kutengeneza mazingira ya makazi na ardhi inayosimamiwa na wizara yake kuwa katika sura itakayomsaidia Mtanzania wa leo na miaka 50 ijayo.

Waziri Silaa aliwataka watumishi wa sekta hiyo kujitahidi katika utoaji huduma bora kwa wateja hasa katika utoaji kauli wakati wa kuwahudumia.

"Mjitahidi majibu mnayowajibu wananchi ili wawe watulivu na subira kwani inawezekana suala unalofanya liko nje ya uwezo wako. Unatakiwa kumwelezea katika lugha ambayo anaweza kuelewa ili akitoka ajue anasubiri kwa muda gani na muepuke njoo kesho, njoo kesho," alisema.

Aliwathibitishia watumishi wa ardhi kuwa wakati wote atakuwa makini kuwalinda lakini wafanye kazi ya kuwasaidia wananchi. Pia Silaa aliwataka watumishi wa sekta hiyo kuhakikisha wanapotoa huduma kwa wananchi basi kwa suala lililofika mwisho lifanyike kwa maandishi ili kuepusha matatizo.

# 'Wateja benki zilizofilisiwa nendeni TCB'

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Bima ya Amana (DIB) imewataka waliokuwa wateja wa benki zilizofilisiwa kwa kukiuka taratibu na kushindwa kujiendesha kwenda Benki ya Biashara Tanzania (TCB) kwenda kuchukua fedha zao zinazokadiriwa kufikia Sh. bilioni 2.9.

Mkurugenzi wa DIB, Isack Kihwili, alitoa rai hiyo jana wakati akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari baada ya kumalizika kwa mafunzo ya siku mbili yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Kihwili alisisitiza kuwa fedha hizo ambazo ni sawa na asilimi 25 ambazo hazijalipwa, ni kati ya Sh. bilioni 11 ambazo zilikuwa zinadaiwa na wateja wa benki hizo tisa baada ya kufilisiwa na serikali kwa kukiuka taratibu.

Alisema kati ya wateja hao ambao wanatakiwa kwenda kuchukua fedha zao TCB, ni wa iliyokuwa Benki ya EFATA Limited (2018) ambao wanadai Sh. milioni 403.

Kihwili alifafanua kuwa wakati benki hiyo ya EFATA ikifilisiwa, wateja wake walikuwa wakiidai Sh. bilioni 1.486 na kwamba wengine walijitokeza kwenda kuchukua na kusalia kiasi hicho.

"Wengi wanaamini benki itarudi, waje kwamba benki ikiishafilisiwa na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) wakishafuta leseni maana yake imekufa kurudi tena haiwezekani," alisisitiza.

Kihwili alisema wateja hao wanatakiwa kwenye TCB au kwenye Ofisi za DIB wakiwa na vielelezo ikiwa ni pamoja na vitambulisho kwa ajili ya kupatiwa fedha zao hizo.

"Wafike kwenye ofisi za TCB, wafanyakazi wapo watawapa ushirikiano na kuwashughulikia, wasiwe na wasiwasi wowote ila wawe na vitambulisho," alisisitiza. Alizitaja benki nyingine zilizofilisiwa na kufutiwa leseni na BoT kwa kushindwa kujiendesha na kukiuka utaratibu kuwa ni Greenland Tanzania Limited, Delphis Bank Tanzania (2003), FBME, Benki ya Wananchi Mbinga (2018), Benki ya Wananchi Meru (2018) na Benki ya Covenant for Women (T) (2018). Nyingine aliitaja ni Benki ya Kagera Farmer's Cooperative (2018).

Kwa mujibu wa Kihwili, DIB imeanzishwa kwa ajili ya kuwalinda wenye amana dhidi ya upotevu wa amana zao katika tukio la kushindwa, kufilisiwa kwa benki au taasisi ya fedha nchini.

Majukumu makuu ya Bodi ya Bima ya Amana (DIF) ni kutathimini na kukusanya malipo ya bima na michango kutoka katika benki na taasisi za fedha nchini.

Mengine ni kuusimamia Mfuko wa Bima ya Amana, kuwalipa wenye amana zao iwapo benki au taasisi ya fedha itashindwa au kufilisika.

Kufanya ufilisi wa benki au taasisi za fedha zilizoshindwa, filisika pale ambapo BoT imeteuliwa.

Faida ya DIB ni kukinga amana katika benki au taasisi wanachama bila gharama kwa wenye amana na kufanya malipo ya amana iwapo taasisi hizo zitashindwa.

HABARI KITAIFA

## Simbachawene: Fanyeni kazi kila kitu kinataka pesa

**Na Lusungu Helela,**
KIBAKWE

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amewataka wananchi kufanya kazi kwa bidii ili kujiingizia kipato na kumudu gharama za maisha.

Amesema ni wajibu wa kila Mtanzania kwa nafasi yake kufanya kazi kwa bidii ili kupata fedha za kumwezesha kumudu huduma muhimu za kila siku katika jamii.

Simbachawene alitoa wito huo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Mbuga katika Jimbo la Kibakwe, Mpwapwa mkoani Dodoma, ikiwa ni ziara yake ya kikazi ya kuzungumza na kusikiliza changamoto zinazowakabili wananchi wa jimbo lake.

"Ukiwa huna fedha ikitokea umeumwa, utashindwa kupata matibabu na kuhatarisha uhai wako, hivyo ni bora kila mmoja wetu akahakikisha anafanya kazi ili apate fedha za kumudu mahitaji muhimu," alisisitiza huku akisema kila mwananchi kwa nafasi yake ni muhimu akahakikisha anajikita katika kuzalisha mali ili kupata fedha.

Alifafanua kuwa hakuna maisha magumu kama inavyodaiwa na watu wengi isipokuwa mahitaji ya fedha yameongezeka kutokana na kukua kwa maendeleo.

Kutokana na hali hiyo, Simbachawene aliwataka wananchi kuacha tabia ya kukaa bila kufanya kazi badala yake waitumie ardhi yenye rutuba waliyojaliwa kuwa nayo kwa ajili ya shughuli za kilimo ili kujikwamua kiuchumi.

Kwa mujibu wa Waziri Simbachawene, maendeleo ni mchakato ambapo kila huduma inayoletwa inahitaji fedha, akitolea mfano kuwa ili mtu aingize umeme katika nyumba yake, anahitaji awe na fedha.

Katika hatua nyingine, Simbachawene aliutaka uongozi wa vijiji vinavyounda Kata ya Mbuga kuunda sheria ndogo ndogo za kupiga marufuku unywaji pombe nyakati za asubuhi ili muda huo utumike katika kuzalisha mali.

Alisema ni aibu kuona vijana hawafanyi kazi wanachowaza ni kunywa pombe kuanzia asubuhi hadi jioni na kusisitiza kuwa sehemu hizo za kuuzia pombe zisiwe za vificho huku akitaka uuzwaji huo uanze kufanyika jioni wakati wananchi wengi wakiwa tayari wameshafanya kazi.



Wazee wa kimila wa jamii ya Kimaasai katika kijiji cha Orkeeswa, wilayani Monduli mkoani Arusha, wakichuna ng'ombe dume aliyechinjwa juzi, aliyetolewa na mmoja wa Malaigwanaan kama faini ya adhabu ya kukutwa na hatia ya kujihusisha kimapenzi na mkwe wake. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Mfumo mpya ununuzi kuongeza uwazi

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma (PPRA), imesema mfumo mpya wa ununuzi (National e-Procurement System of Tanzania - NeST) utaongeza uwazi kwenye zabuni.

Pia mfumo huo umeelezwa kuwa utaondoa mianya ya rushwa na kuimarisha usalama wa taarifa za manunuzi na za watumiaji wa mfumo huo.

Mfumo wa zamani wa Tanzania National Electronic System (TANePS) unatarajiwa kuzimwa mwezi wa kumi na kuanza kutumika mfumo huo mpya ambao umetengenezwa na kusimamiwa na serikali.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Ofisa Mtendaji Mkuu wa (PPRA), Eliachim Maswi, wakati akiwaelimisha wahariri na waandishi wa habari kuhusu mfumo huo mpya na changamoto za mfumo wa zamani.

Maswi alisema serikali iliamua kuanzisha mfumo wake kwani mkataba na kampuni ya Ugiriki ambayo ilitengeneza na kuendesha mfumo wa TANePS unamalizika Desemba 31, mwaka huu.

Alisema miongoni mwa faida za mfumo huo ni kuongeza uwazi katika michakato ya ununuzi wa umma na mfumo umeweka uwezo wa kusajili na kupitisha wazabuni waliokidhi vigezo kutokana na eneo analofanyia biashara.

Mfumo huo, alisema utaondoa uwezekano wa wazabuni wasio na vigezo kuomba kazi wasizokuwa na utaalamu nazo kama ambavyo ilikuwa ikifanyika kwenye mfumo wa zamani, hivyo kupatikana thamani ya fedha kwenye miradi mbalimbali. "Kwa mantiki hiyo wazabuni watakaoweza kuomba kazi serikalini ni wale pekee waliokidhi vigezo vyote vinavyostahili kwani mfumo kwa kiasi kikubwa utakuwa unawachuja wasiostahili," alisema Maswi

Alisema mfumo huo mpya utaweka usawa na utaondoa kabisa vitendo vya upendeleo kwenye zabuni kwani wenyewe utakuwa ukichakata zabuni hizo na kutoa majibu ya mshindi tofauti na mfumo wa zamani.

Maswi alisema mfumo huu mpya utasaidia kuongezeka kwa idadi ya waomba zabuni kutokana na kuwa na uwazi na kutokuwepo kwa vitendo vya rushwa kwani baadhi ya watu waliogopa kuomba wakijua kwamba hawatashinda.

"Kwenye mfumo wa zamani watu walikuwa wakilalamika kwamba anaomba zabuni miaka miwili hapati wanaopata ni wale wale wanaojuana lakini kwenye mfumo huu uwazo utakuwa mkubwa na hakutakuwa na upendeleo kwa hiyo wazabuni wataongezeka kwasababu watakuwa na imani ya kushinda iwapo wataomba," alisema

Pia alisema mfumo utapunguza muda na gharama za uandaaji wa michakato ya zabuni kwa kurahisisha baadhi ya taratibu na kuwezesha upatikanaji wa huduma bora kwa kuhakikisha wazabuni wanaoomba zabuni wanavigezo vinavyotakiwa.

Alisema mfumo mpya ni rahisi kutumiwa na watu wote hata wenye uelewa mdogo wa kutumia teknolojia na kuongeza usalama wa taarifa za ununuzi na watumiaji wa mfumo

Kuhusu changamoto za TANePS, Maswi alisema iwapo serikali ingeendelea na mfumo huo ingeendelea kurithi matatizo yaliyopo sasa ya kuwa na mfumo ambao haukidhi mahitaji ya watumiaji na kwamba kama serikali ingetaka mfumo huo uhuishwe ingetumia fedha nyingi. Alisema teknolojia iliyotumika kwenye mfumo huo wa zamani imepitwa na wakati na mfuo umekuwa na changamoto za kiufundi na kiutendaji na hivyo kupunguza ufanisi na urahisi wa matumizi ya mfumo kwa waomba zabuni.

"TANePS ilikuwa na hitilafu nyingi na hazitatuliwi kwa wakati na mfumo umeshindwa kabisa kulinda usalama wa taarifa za ununuzi na ulicheleweshaa zabuni na wakati mwingine zabuni zingine kufutwa bila sababu," alisema Maswi alisema kwenye mfumo wa zamani walifanikiwa kusajili taasisi nunuzi 865 na mfumo ulisajili wazabuni 37,445 na jumla ya zabuni zilizowasilishwa kwenye mfumo huo tangu uanzishwe zilikuwa zabuni 142,606.

# NEMC yaonya wachimbaji matumizi holela ya zebaki

**Na Said Sindo,** GEITA

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limewataka wachimbaji wadogo na wakubwa kuchukua tahadhari dhidi ya matumizi holela ya zebaki katika shughuli zao.

NEMC imesema uchimbaji kwa kutumia holela zebaki una madhara makubwa kwa jamii na uharibifu wa mifumo ya ikolojia.

Mratibu wa Mradi wa Kudhibiti Matumizi ya Zebaki kutoka NEMC, Dk. Befrina Igulu, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza kwenye maonyesho ya matumizi sahihi ya teknolojia katika kuinua wachimbaji wadogo kiuchumi na kuhifadhi mazingira.

"Tunapaswa kuchukua tahadhari kabla ya athari kutokea ili kukidhi matakwa ya serikali katika kufanikisha azma ya kupunguza uchafuzi utokanao na matumizi endelevu ya rasilimali za maji, udongo na afya za jamii," alisema.

Alisema anatambua kuwa kwa nyakati tofauti katika shughuli zao wamekuwa na mijadala ya namna bora ya kutunza mazingira kwa wachimbaji bila kuathiri shughuli zao ambazo ni nguzo za maendeleo kwa jamii za uchimbaji mdogo.

Dk. Igulu aliwahakikishia kuwa hilo ndilo lengo la serikali linalotekelezwa na NEMC na kuhimiza ushirikiano baina ya wachimbaji hao katika kudhibiti matumizi holela ya kemikali hizo.

"Mafunzo haya yamekuja wakati mwafaka mkizingatia kuwa ongezeko la wachimbaji wadogo nchini litakwenda sambamba na ongezeko la uharibifu wa mazingira na matumizi ya kemikali za zebaki, hivyo yatumieni vyema kudhibiti athari za kimazingira na kibinadamu zinazosababishwa na kemikali hizi," alisema.

Mchimbaji mdogo, Alex Bawazir, alisema elimu waliyoipata kuhusu matumizi sahihi itawasaidia kuokoa mazingira na afya zao na kuahidi kufuata maelekezo muhimu kuepuka madhara yake.

Mkurugenzi wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira kutoka NEMC, Lilian Lukambuzi, alisema wachimbaji wadogo wanahitaji elimu ili kuokoa mazingira na afya zao.

Alisema sekta ya madini ni kubwa inayotumia teknolojia kwenye uchimbaji ambayo inaweza kuwa na athari kwa mazingira kama matumizi ya zebaki yataendelea bila kufuata utaratibu wa kitaalamu.

"Lengo la kuja hapa ni kuwapa elimu wachimbaji wadogo ambao ndiyo watumiaji wa zebaki katika kuchimba madini. Sisi tunamradi ambao tunausimamia wa kudhibiti matumizi holela ya zebaki ili hawa wachimbaji waone kwamba shughuli wanazofanya zinaweza kuathiri vipi mazingira na kuwaelimisha kuhusu teknolojia mbadala wa zebaki," alisema.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera TFF kuzibeba timu za wanawake michuano CAF

**WAKATI** Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), jana jioni ilikuwa ugenini Ivory Coast ikicheza mechi ya kwanza ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (WAFCON 2024) dhidi ya wenyeji, leo wadogo zao, Serengeti Girls (U-17), wanashuka dimbani kucheza mchezo wa kirafiki.

Serengeti Girls itawakaribisha wenzao kutoka Morocco na timu hizo zitarudiana keshokutwa, mchezo huo wa pili ukilenga kutoa nafasi kwa wachezaji wengine kujipima.

Mtendaji Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao, amenukuliwa akisema lengo la kuandaa mechi za kirafiki kwa yosso hao ni kuwajenga na kuwaweka tayari na michezo ya mashindano watakayocheza kuanzia Januari mwakani.

Kidao alisema shirikisho hilo limejipanga kuwaimarisha Serengeti Girls kwa kuwaendeleza pale walipoishia mwaka jana ambapo walifuzu kushiriki fainali za Kombe la Dunia la Wasichana wa umri chini ya miaka 17, kwa mara ya kwanza.

Haya yanayofanyika sasa wakati TFF inaongozwa na Rais, Wallace Karia yanastahili kupongezwa kwa sababu si tu kuweka mikakati ya kuandaa timu, lakini baadhi ya nchi zimejitoa kushiriki mashindano mbalimbali ya soka la wanawake kwa kigezo cha kukosa fedha.

TFF ya sasa imekuwa ikigharamia kambi mbalimbali za timu za wanawake (Twiga Stars, Tanzanite na Serengeti Girls), ambazo hazina wadhamini kwa sababu zinahitaji kupata matokeo chanya ambayo yanaipa heshima taifa letu.

Ni ukweli usifichika ili timu yoyote ifanye vizuri katika mashindano mbalimbali ni lazima kuwapo na maandalizi sahihi, mchezo wa soka hauhitaji miujiza, timu iliyosajili vyema na iliyofanya maandalizi sahihi ndio yenye nafasi kubwa ya kuvuna ushindi.

Uwekezaji katika jambo lolote ndio hupelekea kupatikana matoke chanya, hivyo kinachofanywa na TFF sasa ni cha kupongezwa kwa sababu inahitaji kufikia malengo na si kupeleka timu kwenye mashindano bila ya kuzipa maandalizi yanayostahili.

Ikumbukwe miaka ya nyuma tulishuhudia timu za wanawake zikisafiri kwa njia ya barabara kwa umbali mrefu ili kufika katika kituo cha mashindano, jambo ambalo kwa sasa halipo, timu ikikosa vifaa vya mazoezi, jambo ambalo kwa sasa halipo, hii yote inafanyika kwa sababu TFF inataka kuona malengo yanafikiwa.

Inafahamika timu zinazowania tiketi ya kushiriki fainali zijazo za WAFCON 2024 na Kombe la Dunia (u-17), ni nyingi na nafasi zilizopo ni chache, ili kufikia malengo hayo ni wazi kila nchi inafanya maandalizi na ili TFF ifikie malengo yake, inahitaji ushirikiano kutoka kwa viongozi wa klabu, serikali na wadau mbalimbali.


Tunaipongeza pia TFF kwa kuwa karibu na mabingwa wapya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, JKT Queens kuanzia kwenye maandalizi hadi ilipokwenda kupambana na hatimaye kutwaa taji la Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) na kupata tiketi ya kuuwakilisha ukanda huo kwenye michuano ya Afrika itakayofanyika baadaye mwaka huu nchini Ivory Coast.

Pongezi nyingine zinatakiwa kwenda kwa serikali kwa sababu bila ya kuweka nguvu na mkono wake, mambo haya mazuri huenda yangeendelea kuwa mageni kwa Tanzania, lakini kwa sasa taifa letu limeweza. Pamoja na mafanikio ambayo timu za wanawake wameshapata, TFF haitakiwi kubweteka kwa sababu majirani nao wanahitaji kutimiza ndoto zao kwa kuwafunga na kuwaondoa kwenye mbio za mafanikio.

Ili timu zetu za wanawake ziendelee kuwapa furaha kama ambavyo kaka zao, Taifa Stars walivyofaulu kukata tiketi ya kucheza AFCON mwakani, ni lazima wadau wajitokeze kuwekeza kwa sababu hakuna mafanikio yanayopatikana bila ya kutumia fedha.

Kila la kheri Twiga Stars katika mechi ya marudiano dhidi ya Ivory Coast itakayochezwa Septemba 26, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwangwo

# Mashabiki Simba na Yanga tusisahau Fair Play muhimu

**BAADA** ya beki wa Simba, Henock Inonga kuumia kutokana na rafu mbaya aliyofanyiwa na Haji Ugando wa Coastal Union, nimekuwa nikipita katika mitandao mbalimbali ya kijamii na kusoma maoni ya watu na kugundua bado tuna safari sana kwenye soka letu.

Yaani unakuta mtu anafurahia mchezaji huyo kufanyiwa rafu. Anapoulizwa sababu eti na yeye alishawahi kumfanyia rafu mchezaji, Aboubakar Salum 'Sure Boy' katika mechi ya Ligi Kuu Bara msimu uliopita.

Unaanza kujiuliza kama kila mchezaji aliyewahi kufanya rafu nyuma, basi aendelee kufanyiwa hivyo na yeye siku zote?

Hata alipoumizwa katika mechi ya Ngao ya Jamii baadhi ya mashabiki pia waliona ni sawa tu kwa sababu alishawahi kumchezea 'Sure Boy.'

Nadhani hata akiendelea kufanyiwa rafu nyingine huko mbele ya safari kuna watakaoona sawa tu kwa sababu siku moja alishawahi kumchezea mchezaji fulani kama hivyo.

Baadhi yao wanaoandika hivyo ni watu wenye heshima zao, ambao kwenye jamii wanaheshimika lakini linapokuja suala la Simba na Yanga inakuwa kinyume chake. Inakuwaje mtu afurahie mchezaji kuumizwa kwa sababu yeye alishawahi kufanya hivyo huko nyuma? Yaani kosa moja limhukumu siku zote? Huo ndiyo mpira?

Kwa hiyo ni ruhusa kwa mchezaji yoyote aliyefanya hivyo huko nyuma kuumizwa?

Ukiangalia yote haya utagundua tu ni suala la upinzani wa Simba na Yanga, na kama ikiendelea hivi tunakoelekea ni kubaya, itafikia wakati watu watafurahia mtu akivunjika mguu na kumaliza 'karia' yake ya soka.

Mashabiki wa soka wafikirie jinsi wao wanavyofanya kazi na kupata pesa kwa shida, hivyo hivyo wachezaji nao wapo kazini.

Watu wanaofanya hivi hawana tofauti na wanaofurahia mtu kukatika mkono au mguu, kufukiwa na kifusi au kupatwa na janga lolote unapokuwa kazini.

Je, wao wapo tayari kuwaona wenzao wanafurahia wanapokutwa na majanga kazini?

Ikumbukwe wachezaji hao wapo kazini na wanalipwa ili wahudumie familia, wazazi pamoja na watu wanaowazunguka, hivyo kitendo cha kufurahia kuumizwa ni jambo baya na kwa tamaduni zetu Waafrika tunasema ni mwiko.

Mashabiki wakumbuke Simba na Yanga si maadui ila ni watani wa jadi, hivyo kumwombea mtu mabaya au kufurahia si jambo jema.

Hawa wachezaji si wanachama au mashabiki wa timu, leo yupo Simba kesho Yanga, keshokutwa Azam FC au JKT Tanzania, hivyo kufurahia au kuonyesha kuguswa na kuumizwa kwa mmoja wao kwa sababu si mchezaji wa timu unayoipenda si uungwana hata kidogo.

Hapa mashabiki watakuwa wakipanda bomu litakalokuja kuwalipukia wenyewe kwa sababu hata wachezaji ambao wanafanya vitendo hivyo wakiona kuna watu wanaowasapoti wataendelea navyo.

Kilichopaswa kufanyika ni mashabiki wa timu zote waungane ili kupinga tabia ya baadhi ya wachezaji ambao wao kitu kukamia wanaona ni kuwachezea rafu au kuwaumiza wenzao.

Tumeona Jumatano iliyopita mchezaji wa Yanga, Joyce Lomalisa naye alivyochezewa vibaya na nyota wa Namungo ingawa mwamuzi, Emmanuel Mwandembwa hakuchukua hatua yoyote ya maana kama mwenzake ,Ahmed Aragija alivyoamua.

Hapa sina maana kama Ugando alifanya makusudi kucheza rafu ile, la hasha, ila kwa miaka ya hivi karibuni kumekuwa na baadhi ya matukio ya wachezaji kuchezeana rafu mbaya.

Nadhani hii inatokana na waamuzi wengi kutochukua hatua stahiki kama alivyofanya Aragija.

Kumekuwa na tabia ya wachezaji kukamiana, kutolindana, lakini waamuzi wetu wamekuwa hawachukui hatua kiasi kwa sasa wameshazoea na wakilimwa kadi wanaona wanaonewa.

Ukiangalia wenzetu huwezi kukuta aina ile ya uchezaji na kupamiana hovyo na rafu yoyote moja tu mbaya inaweza kukutoa uwanjani.

Wao wanataka mchezaji mwenye uwezo na kipaji aonyeshe bila kuogopa kuchezewa rafu za hivyo na wenzake kwa sababu mashabiki wamelipa fedha zao kwa ajili ya kuangalia soka na si rafu.

Baadhi ya wachezaji wa wanaocheza Ligi Kuu wanashindwa kutofautisha kucheza mpira wa nguvu na kucheza rafu.

Waamuzi sasa wanatakiwa wawe macho ili kukomesha matukio hayo huku pia makocha wao wakitakiwa kuwakumbusha kuachana na matukio hayo.

# Wanaume kupewa darasa kuongeza ushiriki wa wanawake katika uongozi

**Na Yasmine Protace**

KITUO cha Taarifa na Maarifa Kivule kinatarajiwa kutoa elimu kwa wanaume ili waachane na masuala ya mfumo dume unaofanya wanawake wengi kushindwa kushiriki katika nafasi za uongozi.

Erick Andeson, katibu wa kituo hicho, aliwaambia waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana kuwa wanatarajia kutoa elimu hiyo kwa lengo la kuongeza idadi ya wanawake katika nafasi za uongozi na ushiriki wao kiuchumi.

Andeson alisema mfumo dume umekuwa unachangia wanawake kushindwa kushiriki katika nafasi za uongozi na ngazi za uamuzi.

"Baadhi ya wanawake ukiwahoji sababu za kushindwa kujitokeza katika kugombea uongozi, wanasema waume zao huwaachia majukumu ya nyumbani kuyafanya na kukosa muda wa kushiriki katika masuala ya kugombea uongozi," alisema.

Alisisitiza majukumu ya nyumbani kwa kiasi kikubwa yamekuwa yanatekelezwa na wanawake huku wanaume wakiwa hawatoi mchango wowote, hivyo kulifanya kundi hilo kushindwa kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Katibu huyo alisema kuwa baada ya kubaini hilo wameona kuna haja kutoa elimu kwa wanaume ili kuwaelimisha athari za mfumo dume.

Pia alisema wanatarajia kutoa elimu kwa wafanyabiashara wanawake wanaofanya biashara zao barabarani na magengeni, ili watafute vizimba sokoni na kuanzisha umoja kwa ajili ya kupata fursa.

Alibainisha kuwa baadhi yao wamekuwa hawana umoja na mshikamano zaidi ya vikundi vya kuweka na kukopa (Vikoba) ambavyo hata hivyo, wakiachana umoja unakuwa haupo tena.

Alisema changamoto za wanawake wanaoishi Kivule zinahusiana na tatizo la mfumo dume, mila na desturi kandamizi, rushwa ya ngono, elimu duni ya uongozi, majukumu ya kifamilia na uchumi duni wa kaya.



Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Marprisca Mahundi (kulia), akimkabidhi cheti cha ushiriki Mkuu wa Kitengo cha wateja Binafsi na Biashara wa benki ya KCB, Juma Abdul wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mara, wilayani Mugumu juzi. Siku hiyo, ililenga kuwakusanya wadau wa mazingira na kufanikisha kupanda miti 6,000 ili kuendeleza Bonde la Mto Mara. Katikati ni Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda na (kushoto) ni Katibu Mkuu wa Kamisheni ya Bonde la Mto Mara, Dk. Masinde Bwire. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Magonjwa yasioambukiza tishio, serikali kufanya utafiti kuyakabili

**Na Romana Mallya**

SERIKALI kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO) katika kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza, inatarajia kutoa utafiti mpya mwishoni mwa mwaka huu kuhusu idadi ya watu wanaokula inavyopaswa, wenye magonjwa ya moyo na kisukari.

Utafiti wa magonjwa yasiyoambukiza (Step Survey) kwa mara ya mwisho ulifanyika mwaka 2012 na kuonesha ulaji wa mboga na matunda Tanzania uko chini. Katika Watanzania 100, watatu mpaka wanne ndiyo hula.

Vilevile, utafiti huo ulionesha matumizi ya pombe katika watu 100 walikuwa ni asilimia 29, tumbaku ni asilimia 15.9, tabia bwete na uzito uliozidi ni asilimia 26.

Kaimu Meneja Mpango wa Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya, Valeria Millinga, alibaisha hayo juzi katika kongamano kuhusu wagonjwa wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza likiwa na kaulimbiu ya 'Sauti Zao, Maoni yao.'

Akizungumzia kuhusu utafiti huo mpya, Valeria alisema unafanywa na serikali kupitia Wizara ya Afya, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na WHO na utahusisha pia idadi ya wanaofanya mazoezi.

Alisema utawezesha serikali kupanga afua mbalimbali na udhibiti wa hali iliyoko sasa.

Alisema urahisi wa maisha na teknolojia unawafanya watu wengi kukaa zaidi kwenye viti kuliko kushughulisha mwili na kusababisha watu kuwa katika hatari ya kupata magonjwa yasiyoambukiza.

"Hali hii ya magonywa yasiyoambukiza takwimu za Wizara ya Afya kwa mwaka 2020/21, tulikuwa na wagonjwa milioni 3.4, mwaka jana 2022 walikuwa milioni 3.5. Tuna jumla ya wagonjwa waliotambuliwa ni 412,000 ongezeko la asilimia 12 kwa mwaka mmoja," alibainisha. Valeria alisema ugonjwa unaongoza ni shinikizo la juu la damu, ukifuatwa na kisukari.

Kuhusu ugonjwa wa saratani, alisema kila mwaka Tanzania huwa na visa vipya kwa wanaogundulika ambao idadi yao ni 40,464. Kati yao, asilimia 25 ni wenye saratani ya malango wa kizazi, asilimia 9.9 ni saratani ya matiti na asilimia 8.8 saratani ya tezi dume.

Alisema takwimu zinaonesha kila mwaka watu 26,945 hupoteza maisha na jukumu la serikali ni kuhakikisha kwamba mara baada ya watu kupata matibabu wanaendelea kuishi.

Alisema Tanzania inaongoza kati ya nchi tano duniani zenye wagonjwa wa selimundu ikiwa na wastani wa mtoto mmoja mwenye shida hiyo katika kila watoto 100. Huzaliwa nayo na kusababisha asilimia 15 ya Watanzania kuishi na vinasaba vya ugonjwa huo.

"Katika watoto 100 tunaowapata, watoto 70 mpaka 90 hufariki dunia kutokana na selimundu kabla ya kufikia miaka mitano.

"Katika kukabiliana na tatizo, tumezindua huduma ya kupima ili kubainika mapema na inafanyika baadhi ya mikoa hasa inayoonekana kuwa na idadi kubwa," alisema.

Kuhusu ugonjwa wa afya ya akili, ofisa huyo alisema kuwa mwaka 2022, walitoa huduma kwa wagonjwa 260,000, wengi wao ni wenye kifafa, sonona na wanaotumia dawa za kulevya.

"Tanzania ndiyo nchi ambayo kuna hali ya juu ya watu wanapata matatizo ya afya ya akili. Utafiti wetu unaonesha watu wenye umri kuanzia miaka 13 mpaka 17 wenye umri balehe, angalau 12 kati ya watu 100 wamepata hisia ya kutaka kujiua. Katika kila watu 100 wenye tatizo hilo, 10 walijaribu kukatisha uhai wao," alisema.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# Wakulima wadaiwa kuvamia makazi ya wafugaji kwa bunduki, waua ng'ombe

**Na Mwandishi Wetu**

MGOGORO kati ya wafugaji na wakulima katika Kijiji cha Lembapuli, Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara umechukua sura mpya baada ya wakulima kudaiwa kuvamia makazi ya wafugaji na kushambulia mifugo kwa risasi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya waathirika wa tukio hilo wamedai lilifanyika usiku wa kuamkia jana. Watu wanaodaiwa wakulima walivamia makazi na kushambulia mifugo kwa risasi.

Mmoja wa waathirika wa tukio hilo, Sanyakwa Kapande, alidai kuwa watu hao walivamia nyumba yake kisha kuvunja milango na kuvamia zizi la ng'ombe. Baadaye walishambulia kwa risasi ng'ombe kadhaa.

"Wengine waliingia katika zizi la ng'ombe wakaenda kupiga risasi ng'ombe 10. Kati yao, mmoja amekufa wengine wamejeruhiwa vibaya. Siidhani kama watapona kwa sababu wamepigwa risasi tumboni na kuvunjwa miguu," alidai Kapande.

Alipoulizwa chanzo cha tukio hilo, Kapande alidai ni mgogoro wa ardhi kati ya wafugaji na wakulima, ulioibuka tena baada ya kusuluhishwa na mamlaka ya kijiji.

"Nahisi shida ni mgogoro wa ardhi, huko nyuma tulisuluhishwa na kuambiwa wafugaji tulipe fidia baada ya ng'ombe wetu kuvamia mashamba, tulilipa ukaisha, lakini tunashangaa wamerudi tena," alidai Kapande. Tilian Naisendu, mkazi mwingine wa eneo hilo, alidai "... hapa kuna mgogoro wa muda mrefu sana, watu wanagombea mipaka. Serikali ilikuja kutafuta chanzo tatizo wakaja kupima na kugawa maeneo ikawaondoa wakulima, lakini wakulima hawataki kuondoka maeneo waliyotengewa wafugaji."

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, George Katabazi, alipotafutwa kwa ajili ya kupata ufafanuzi wa tukio hilo, alisema kuwa walikuwa wanafanya uchunguzi kujua chanzo chake.

"Nipo kwenye kikao, lakini taarifa hizo ni za kweli. Eneo hilo limekuwa na mgogoro wa ardhi kati ya wakulima na wafugaji. Taarifa za awali zinadaiwa kuwa ng'ombe tisa wamejeruhiwa na mmoja kuuawa," alijibu Kamanda Katabazi katika ujumbe mfupi wa maandishi alipowasiliana na mwandishi wa habari hizi.



Mratibu wa Kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia Bariadi, Anthony Mlelwa akitoa elimu kuhusu malengo ya kampeni hiyo kwa wanafunzi wa shule ya sekondari Biashara, Bariadi Mjini mkoani Simiyu jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vijana waonywa kutumika kuvuruga amani

**Na Beatrice Shayo**

NAIBU Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Ojambi Masaburi, amewataka vijana katika nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu kuacha kutumika katika vitendo vya uhalifu na uvunjifu wa amani kwa kuwa vina athari kwao na nchi zao.

Meya Masaburi aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipopokea matembezi ya kuadhimisha Siku ya Amani Duniani yaliyofanywa na vijana kutoka nchi za Maziwa Makuu ambazo ni Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Uganda, Rwanda na Tanzania.

Alisema ni muhimu vijana kuacha kushabikia mambo yasiyokuwa ya msingi ambayo yanaweza kuleta machafuko na uvunjifu wa amani na kuwataka wayaseme yale mema ya serikali na kutoa ushauri pale inapohitajika kufanya hivyo.

"Bila kuwa na amani hatuwezi kuwa na maendeleo. Amani inapotea tunapoteza ndugu, baba, mama na watoto pamoja na watu wenye mahitaji maalum kwa maana ya walemavu.

"Kwa mujibu wa takwimu za dunia, zaidi ya vijana bilioni 1.4 duniani wanaishi katika maeneo au nchi zenye mchafuko, na wanawake 600,000 wanaishi kwenye nchi zenye machafuko, takwimu hizi siyo nzuri," alionya.

Ofisa Maendeleo ya Vijana wa Jiji hilo, Happness Joackim, alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuhimiza vijana hususani walioko katika nchi ambazo zinazungukwa na maziwa makuu, kulinda na kutunza amani za nchi zao.

Aliwataka vijana wasikubali kujiingiza katika machafuko ya kikabila, kisiasa au ya nchi na nchi kwa sababu kwa kufanya hivyo kutaleta matatizo mengi ikiwamo kupoteza ndugu, jamaa na marafiki.

Pia aliwakumbusha kwamba nchi inapoingia katika mgogoro, kundi kubwa linaloathirika ni watoto, wanawake, watu wenye ulemavu na vijana wenyewe.

"Amani tuliyonayo katika nchi zetu ina maana kubwa na Tanzania tuna amani, vita vinavyotokea katika nchi zingine jirani, zinasababisha athari huko na hapa tunapokea wakimbizi, ni muhimu tulinde na kutunza amani za nchi zetu," alisisitiza.

Mratibu wa Taifa wa Mtandao wa Vijana wa Nchi za Maziwa Makuu kuhusu amani na utulivu, Jimmy Luhende, alisema kongamano hilo la siku tatu, limewakusanya vijana kujadili mambo mbalimbali ikiwamo kupanga mijadala ya kumaliza migogoro katika nchi zao na kudumisha amani.

Alisema tofauti zinapotokea ikiwamo kupeleka majeshi, kutunishiana misuli katika nchi hizo za maziwa makuu, haziwezi kuleta amani wala suluhisho.

Katibu wa Asasi ya Vijana Youth VDT, Nicholus Luhende, alisema kwa mara ya kwanza kongamano hilo lilianzia Congo, kisha likafanyika Kigali, Uganda na sasa Tanzania kwa lengo la kuwakutanisha vijana kutoka nchi hizo kujadili masuala ya amani.

"Nchi ambazo zinatuzunguka Tanzania zimekuwa na changamoto mbalimbali katika masuala ya amani, hivyo kongamano hili limetupa nafasi ya kukaa pamoja na kujadili, kwa kuwa kupitia maongezi tutatatua matatizo yaliyopo," alisema.

# GGML yatoa vifaa tiba kuboresha afya Geita

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

KATIKA jitihada za kuendelea kuboresha sekta ya afya mkoani Geita, Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imetoa msaada wa vifaa tiba kwa Halmashauri ya Wilaya ya Geita na Halmashauri ya Mji wa Geita.

Ni mwendelezo wa mikakati ya kampuni hiyo kudhibitisha dhamira yake katika uwajibikaji kwa jamii.

Msaada huo wenye thamani ya Sh. milioni 260, unajumuisha vitanda 17 vya hospitali, vitanda vitano vya uchunguzi wa kitabibu, majokofu maalum ya kukusanya damu na magodoro.

Kampuni hiyo pia imetoa vifaa maalum vya uchunguzi wa via vya uzazi kwa mwanamke, viua wadudu, majokofu ya kuhifadhi maiti, vifaa vya upasuaji, mashine za kufulia na darubini.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo jana mkoani Geita, Mkuu wa Wilaya ya Geita, Kanali Boniphace Maghembe, aliishukuru GGML kwa ukarimu wao kwa jamii inayozunguka migodi yao.

"Ni furaha yangu kutambua kuwa tangu GGML ianze kazi hapa Geita, wameshirikiana kwa karibu na serikali kutekeleza miradi kadhaa ya afya hususan ujenzi wa zahanati na vituo vya afya," alisema.

Meneja Mwandamizi anayesimamia uhusiano endelevu wa kijamii kutoka GGML, Gilbert Mworia, alisisitiza umuhimu wa huduma bora za afya katika kufikia Lengo Na. 3 la Umoja wa Mataifa la Maendeleo Endelevu, ambalo linalenga katika kuhakikisha maisha ya afya na kukuza ustawi kwa wote.

"Lengo la 3 la Maendeleo Endelevu ni miongoni mwa Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa mwaka 2015, na GGML imejizatiti katika kuboresha afya na ustawi wa watu," alisema.

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2000, GGML imeboresha ustawi wa jamii inayozunguka mgodi kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa ikiwamo afya, elimu, maji, barabara na miradi ya kiuchumi.

GGML pia imeboresha upatikanaji huduma bora za afya mkoani Geita kupitia mipango mbalimbali, si tu kwa msaada wa vifaa tiba, bali pia kupitia ujenzi wa zahanati na vituo vya afya.



# Machifu wahimizwa utatuzi wa migogoro

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

SERIKALI wilayani Ikungi mkoani Singida imesema viongozi wa kimila, wakiwamo machifu, wanayo nafasi kubwa ya kuisaidia serikali kupunguza migogoro mbalimbali kama ya ardhi na ndoa inayojitokeza katika jamii badala ya kusubiri hadi ifikishwe mahakamani.

Ofisa Tarafa ya Mungaa, William Swai, alisema hayo jana alipomwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Thomas Apson, kwenye sherehe za kutimiza mwaka mmoja wa chifu Thomas Mgonto wa kabila la Waheju zilizofanyika katika kijiji cha Siuyu, wilayani hapa.

Alisema serikali imeendeleza mila na desturi na kuweka machifu kwenye koo kwa sababu zipo mila na desturi katika baadhi ya makabila kama zikizingatiwa kuna uwezekano wa kumaliza migogoro midogo na mikubwa kwenye jamii pasipo kuifikisha mahakamani.

"Mfano suala la kumiliki ardhi viongozi wa kiserikali wanapoamua wanatumia sheria ya kiserikali ambapo kunakuwa na uwezekano wa kupoteza haki ya mtu lakini anapotokea kiongozi wa kimila kama chifu akaita wale wote wanaogombana kesi inaisha bila kuwepo uhasama kuliko inapopelekwa mahakamani. Huko anayejua kuongea vizuri ndiye anapewa ushindi, hivyo inamalizika kwa uhasama," alisema.

Aliongeza kuwa maana ya kuwapo machifu ni kuwezesha kutunza kwa uangalifu kila mmoja apate haki yake, hivyo viongozi wa kimila wanahitajika katika ulinzi wa watoto, vijana na wazee.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, kuna wakati vijana wanakosa hata nidhamu kwa watu wazima hivyo machifu wakitumia mamlaka zao watakomesha maadili mabovu kwa jamii.

Chifu Mgonto alikemea mmomonyoko wa maadili katika jamii likiwamo suala la ushoga na kusisitiza kuwa katika eneo lake la utawala pasiwapo na mtu yeyote ananayeshabikia ushoga kwani mambo hayo ni kinyume cha maadili ya kitanzania.

"Mila za kigeni za ajabu zinatuletea mambo ya ushoga, nalikemea hili nasema kama chifu asiwepo mtu yeyote ambaye atashabikia ushoga na kuanzia sasa laana imeshatupwa kwa yeyote atakayejihusisha na ushoga katika himaya yangu," alisema.

Mgonto aliwataka wananchi katika kipindi hiki cha kuelekea msimu wa mvua wananchi wajiandae kuanza kutayarisha mashamba kwa ajili ya kilimo ili kukabiliana na balaa la njaa.

Pia alisisitiza suala la wazazi kuwapeleka watoto kwenda kusoma kwani serikali inajenga shule nyingi ili kutoa fursa kwa watoto wengi kusoma kwa ajili ya kuwa viongozi wa baadaye watakaoliongoza taifa hili.

# Jafo ashtukia usafirishaji wa chuma chakavu nje bila vibali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, amebaini kuwapo kwa wafanyabiashara wasio waaminifu wanaokiuka Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na kanuni zake kwa kusafirisha nje ya nchi chuma chakavu bila vibali.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Dk. Jafo alisema hivi karibuni kumekuwapo na taarifa za usafirishaji wa aina mbalimbali za chuma nje ya nchi huku katika kipindi cha Machi hadi Septemba, mwaka huu, ofisi yake ikiwa haijatoa kibali cha kusafirisha chuma dongo.

"Hivyo ni dhahiri kuwa kuna baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu ambao wanakiuka matakwa ya sheria.

Ikumbukwe kuwa kupitia usafirishaji wa taka hatarishi nje ya nchi kuna tozo na kodi zinapaswa kulipwa, hivyo kusafirisha bila kibali ni kuikosesha mapato serikali," alisema.

Aidha, alisema serikali imeweka mkazo mkubwa katika suala la uwekezaji wa ndani kwa lengo la kuzalisha ajira na kukuza uchumi.

"Usafirishaji wa bidhaa mbalimbali za chuma chakavu kikiwamo chuma dongo nje ya nchi kiholela na kusikofuata utaratibu kunaweza kusababisha upungufu wa malighafi kwenye viwanda vinavyotumia malighafi za aina hiyo hapa nchini kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zikiwamo ndoo na mabomba ya chuma,"alisema.

Aliagiza mamlaka za udhibiti zilizoko kwenye maeneo ya mipaka mbalimbali nchini kuhakikisha shehena yoyote ya taka hatarishi ikiwamo chuma dongo inayosafirishwa nje ya nchi, inafuata masharti ya kanuni za udhibiti na usimamizi wa taka hatarishi za mwaka 2021 ikiwamo kibali kinachotolewa na Waziri mwenye dhamana ya mazingira.

"Naelekeza NEMC (Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira) kusimamia na kushirikiana na vyombo na mamlaka zote za udhibiti zilizopo mipakani katika utekelezaji wa maelekezo haya,"alisema.

Alitoa rai kwa wananchi na wafanyabiashara wanaojihusisha na biashara ya taka hatarishi hapa nchini kuzingatia matakwa ya sheria ya mazingira na kanuni zake.

"Tahadhari inatolewa kwa yeyote anayejishughulisha na shughuli za kukusanya, kuhifadhi, kusafirisha ndani ya nchi, kuingiza nchini, kusafirisha nje ya nchi na kupitisha nchini taka hatarishi bila kibali, atakuwa ametenda kosa la kisheria na atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri akipanda juu ya tangi la maji kwa ajili ya kulikagua alipotembelea mradi unaotekelezwa na Mamlaka ya majisafi na mazingira mjini Dodoma (DUWASA), eneo la Nzuguni, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Shekhe awaangukia wazazi ulinzi watoto

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHEKHE wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, amewaomba wazazi na walezi kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili kwa kutoa taarifa ili hatua za kisheria zichukuliwe badala ya kuwa sehemu ya kuwaficha watu wanaofanya vitendo hivyo.

Ushauri huo aliutoa jana alipokuwa akizungumza na wazazi, walezi, yatima, wajane na wanaoishi katika mazingira magumu kwenye chakula cha pamoja kilichoandaliwa na Jumuiya ya Wanawake wa Kiislamu Tanzania (JUWAKITA) wilaya ya Dodoma.

Alizungumza hayo katika hafla hiyo kwenye Msikiti wa Ghaddafi, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Sikukuu ya Maulidi ambayo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan. Sikukuu hiyo kitaifa itafanyika mkoani Dodoma. Shekhe Rajabu alisema vitendo vya ukatili vimekuwa vikikithiri kila kukicha maeneo mbalimbali huku baadhi vikifanywa na wazazi wenyewe na hata watu wa karibu ambao wanategemewa na jamii kuwa sehemu ya kuwajenga watoto katika malezi bora.

"Hapa naomba niseme na nisisitize kuwa hivi sasa dunia imeharibika sana, hivyo niwaombe wazazi na walezi walindeni hao watoto tutadaiwa mbele ya Mwenyezi Mungu, lazima tuwe waangalifu jengeni tabia ya kuwafuatilia watoto kila wanapotoka shule ili mzitambue changamoto zao," alisema.

Katibu wa JUWAKITA Wilaya ya Dodoma, Zabibu Ally, aliziomba taasisi na mashirika ya kidini kuzikumbuka jamii zilizosahaulika katika kupata mahitaji yao muhimu ikiwemo huduma za kiafya, chakula elimu, maji na mavazi. Alisema jamii hiyo yenye uhitaji bado inakabiliana na changamoto kubwa, hivyo mashirika na taasisi na watu binafsi wanatakiwa kuzisaidia ili kuondokana na hali wanayokabiliana nayo ikiwamo ya kukosa mahitaji muhimu.

Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) wilaya ya Dodoma, Bashiru Omary, aliziomba taasisi zote za dini ya Kiislamu kuwa na moyo wa kujitoa kwa watu wenye kuhitaji mahitaji muhimu kama alivyofanya Mtume Muhammad ambaye alijitoa kwenye maisha yake ya kuwajali watu.

Alisema mbali na yatima na wajane, bado kuna makundi mengine ambayo yanahitaji kusaidiwa kama vile wagonjwa, wafungwa na vituo vya kulelea Watoto. Alisema kote huko kunahitajika misaada, hivyo akawaomba wahisani kujitoa kwa moyo wa upendo kwa kuwafikia na kuwasaidia mahitaji mbalimbali.





# Waziri asisitiza umuhimu vijana kulinda amani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema serikali ya Muungano na ile ya Zanzibar, zinajitolea kuwawezesha vijana kutambua kwamba wao ni sehemu muhimu katika utekelezaji wa maendeleo endelevu.

Aliyasema hayo jana wakati wa madhimisho ya Siku ya Amani Duniani yaliyofanyika katika ukumbi wa Shekh Idrisa Abduli Wakil, Kikwajuni, Zanzibar.

Soraga alisema serikali inatumbua mchango muhimu wa vijana katika amani na mikakati mbalimbali ya serikali inahakikisha kwamba vijana wanaendelea kupatiwa uwezo zaidi.

Alisema katika kutambua umuhimu wa amani, serikali imejikita katika kuhakikisha vijana wanapatiwa elimu juu ya kutunza jambo hilo.

Alisema serikali ya Tanzania inajitahidi kuweka mazingira yanayoruhusu ujasiriamali na uundaji wa ajira kwa kusaidia biashara ndogo na za kati, lengo ni kuongeza uwezo wa vijana kuwa waendeshaji wa ukuaji wa kiuchumi.

"Kipato ni sehemu muhimu sana katika kuhakikisha kwamba vijana wetu hawajihusishi na vitendo vya uvunjaji amani," alisema.

Alisema ushirikishwaji wa vijana katika utunzaji wa mazingira na uchumi wa bluu ni moja ya jitihada zinazochukuliwa na serikali ili kulinda mazingira na kuhifadhi rasilimali za asili kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Ofisa Kiongozi wa Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa Tanzania, Shabnam Mallik, alisema umoja wa mataifa uko mstari wa mbele katika kuhimiza umuhimu wa kutunza amani na ndio msingi wa maendeleo kwa taifa lolote.

Alisema ofisi ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa hivi sasa ina kazi kubwa katika kuzifahamisha nchi juu ya ongezeko la joto katika mataifa yao na hiyo imekuwa changamoto.

# Wanafunzi walia ukosefu wa madaftari

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Kijini, mkoa wa Kaskazini Unguja, wameiomba serikali kuharakisha upatikanaji wa madaftari ya wanafunzi baada ya kukosekana kwa ajili ya kuandika kazi wanazopewa shuleni.

Wakizungumza mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, alipokuwa akisikiliza kero za wananchi wa vijiji vya Kijini na Mbuyu Tende, Matemwe mkoani humo. Walisema hawana madaftari ya kuandika notisi.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kilio chetu kikubwa sisi wanafunzi wa Shule ya Msingi Kijini hatuna madaftari. Tunashindwa kuandika kazi zetu za shule na kutokana na umaskini uliopo kijijini petu, wazee wetu hawana fedha za kutununulia madfatari," alisema Hidaya Khamisi, mwanafunzi wa darasa la tano wa shule ya Kijini.

Mwanafunzi huyo alisema daftari moja ambalo bei yake ni Sh. 800, kijijini hapo linauzwa Sh. 1,200 na kwamba wazazi wao hawana uwezo wa kumudu gharama za daftari.

Aidha, wanafunzi hao walieleza tatizo la walimu kuchelewa kufika shuleni kwa wakati kutokana na ubovu wa barabara na shida ya usafiri wa umma unaofika kijijini hapo.

Vijiji vya Kijini na Mbuyu Tende vilivyoko katika jimbo la Matemwe, mkoa wa kaskazini Unguja, ni miongoni mwa vijiji vilivyoko nyuma kimaendeleo na baadhi ya huduma muhimu hazijafika ikilinganishwa na vijiji vingine.

Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule hiyo, Isack Mashimba Sabuni, alisema shule hiyo imekosa mgawo wa madaftari tangu mwaka jana na hawana madaftari ya kuwapatia wanafunzi.

Baada ya kusikiliza kero hizo, Ayoub alimpigia simu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu Zanzibar, Khamis Ali Said, ili kupata ufafanuzi wa changamoto hiyo.

"Hii ni changamoto kwa sababu katika mkoa wangu, wanafunzi wataendelea kufeli kwa sababu ya uwezo mdogo wa wazazi. Hawana uwezo wa kununua madaftari kwa sababu mzazi mmoja ana wastani wa watoto 10. Sasa atawanunulia wangapi?"alihoji wakati akizungumza na katibu mkuu kwa njia ya simu huku wananchi wakisikiliza maelezo yake.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuendeleza azma ya Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Abeid Amani Karume, ya elimu bure bila malipo, mwaka 2012 chini ya uongozi wa Rais Mstaafu, Dk. Ali Mohamed Shein, alitangaza kuwa serikali itagharamia mahitaji yote ya elimu yakiwamo madaftari na wizara yenye dhamana ya elimu ndiyo itakayosimamia usambazaji wa viandikwa hivyo kwa shule zote za serikali.

Akitoa ufafanunuzi wa changamoto hiyo ya ukosefu wa madaftari Katibu Mkuu Said alikiri uwapo wa uhaba wa madaftari na wizara yake imesita kusambaza madaftari tangu mwaka jana.

Alisema uhaba wa madaftari umetokana na uwezo mdogo wa uzalishaji wa wakala wa serikali wa uchapishaji na kwamba wizara inategemea madaftari kutoka katika kiwanda cha wakala wa serikali.

Said alisema serikali ilitenga bajeti ya Sh. bilioni moja kwa wizara ya elimu kwa ajili ya gharama za uchapishaji wa madaftari kwa shule zote za serikali lakini kiwanda hicho kilishindwa kuzalisha madaftari ya kutosha.

Katibu mkuu huyo alisema katika mwaka huu wa fedha tayari imeshatenga bajeti kwa ajili ya uchapishaji wa madaftari na mwakani madaftari yatasambazwa katika shule zote.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Hamza Johari (wa tatu kulia), akibadilishana nyaraka na Simon Masike wa Kampuni ya Indra Avitech, baada ya kutiliana saini mkataba wa kandarasi ya utekelezaji wa mradi wa mfumo wa usimamizi na utoaji wa taarifa za anga wenye thamani ya Sh. Bilioni 9, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hemed abainisha sababu kumpa mwekezaji uendeshaji bandari

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeikabidhi kampuni ya African Global Logistics (AGL) ya Ufaransa kusimamia huduma za uendeshaji wa bandari ya Zanzibar ili kurahisisha upatikanaji wa huduma bora kwa wafanyabiashara na wananchi.

Hemed aliyasema hayo jana alipokutana na wadau wa bandari wakiwamo mawakala wa ushushaji na upakiaji wa mizigo, wamiliki wa meli na majahazi pamoja na wafanyabiashara katika kutathmini utendaji na uendeshaji wa shughuli za bandari.

Alisema serikali ina dhamira njema ya kuleta mabadiliko ya kiutendaji katika sekta ya uchukuzi hususan bandari kwa lengo la kuleta ufanisi wa huduma.

Kwa mujibu wa Hemed, lengo la kupewa mwekezaji kuiendesha bandari ya Zanzibar ni kujenga nidhamu hasa katika ufanyaji kazi na kuwaondolea usumbufu wadau wa bandari jambo ambalo litaongeza mapato kwa serikali na kuwapunguzia gharama za bidhaa wananchi.

Makamu huyo aliwataka wadau wa bandari kukubaliana na mabadiliko yatakayojitokeza baada ya kuanza kazi kwa AGL na kuhakikisha kuwa serikali kupitia Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) linafanya kazi na muwekezaji huyo kwa kumpa miongozo ili kufanikisha utendaji wake.

Aidha aliwahakikishia mawakala na wadau wa bandari kuwa changamoto ya huduma za fedha na mfumo wa malipo unaotumika sasa zitafanyiwa kazi kwa haraka ili kuenda sambamba na azma ya serikali.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Muhamed, alisema ili nchi ipige hatua kimaendeleo na uchumi uzidi kukua na kuimarika lazima kuwapo na ufanisi katika utendaji kazi hasa katika sekta muhimu kama bandari.

Kwa mantiki hiyo, alisema kuwapo kwa mwekezaji katika bandari ya Zanzibar kutaleta ufanisi mkubwa wa kazi na kuondoa tatizo la kusuasua kwa utendaji kazi na malalamiko yaliyokuwapo kwa muda mrefu.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema kuna haja ya kutolewa elimu kwa wadau na wananchi katika utoaji wa huduma za bandari.

Alisema wako baadhi ya wafanyabiashara wameanza kupandisha bei za bidhaa kwa kisingizio cha kupanda kwa tozo na kodi na kusema yeyote atakaebainika kufanya hivyo, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI SEPTEMBA 23, 2023




# SIRI NZITO

IMEELEZWA mgogoro kati ya wanamuziki Abigail Chamangwana maarufu kama Abby Chams na Marioo ni zaidi ya ugomvi unaojulikana na wengi.

Imeelezwa kuna kila dalili kwamba mgogoro kati ya wasanii hao haukutokana na kazi kama wanavyoeleza wenyewe, bali ni msimamo mkali wa Abby Chams katika suala la mapenzi.

Hivi karibuni Abby Chams ameweka wazi kwamba hajawahi kukutana kimapenzi na mwanaume katika maisha yake na hataendelea kujitunza.

Wadadisi wa masuala ya burudani wamesema huenda msimamo huo ndiyo chanzo kikuu cha wanamuziki hao kutoelewana.

Wasanii hao wawili wamekuwa kwenye bifu baada ya Marioo kumchomoa kiaina Abby Chams katika ngoma yao ya pamoja 'Love Song' na badala yake akamshirikisha Ali Kiba.

Baada ya ngoma hiyo ya Mario na Ali Kiba kutambulishwa rasmi, watu waliiweka mtandaoni ngoma halisi ambayo waliimba Marioo na Abby Chams.

Wachambuzi hao wanaeleza kauli hiyo ya Abby Chams kuhusu msimamo mkali katika suala la mapenzi, inaonyesha wazi ndiyo iliyosababisha wawili hao kutoelewana.

"Tunajua mambo yanayoendelea katika sekta ya muziki, haiwezekani watu wakafanya kazi pamoja halafu kesho akaenguliwa na kuwekwa mtu mwingine. Hapa kuna kitu zaidi na wanachokieleza kwa umma wanatakiwa kusema ukweli," amesema Sadiki Msenembo.

Amesema suala la migogoro ya kimapenzi kwa wasanii duniani kote ni jambo la kawaida, na wakati mwingine wanajengeana chuki endapo mmoja ataonekana hayuko tayari.

BASI SAWA

## Baba levo unachosema ni kweli?



MWANAMUZIKI na mchekeshaji Baba Levo, amesema msanii mwenzake Mwijaku amesababisha kurudisha milioni 37 baada ya kugundua watafanya kazi pamoja.

Amesema Mwijaku huwa habadiliki kitabia na hata kwa mtu anayempatia kula yeye atamsema vibaya.

"Nimerudisha pesa hizo za kampuni ambaye alitaka nifanye nao kazi baada ya kugundua Mwijaku naye amesaini kwa nyakati tofauti," amesema.

## M King Son 'ambamba' Tundaman

KUTOKA nchini Marekani, msanii wa kizazi kipya mwenye asili ya Kongo, M King Son, ameendelea kufanya vizuri baada ya kuachia kolabo yake na mkongwe Tundaman.

Akizungumza na BT, M King Song, amesema wimbo huo unaitwa 'Amenibamba' unafanya vizuri kwenye chati za muziki Afrika Mashariki na kwenye majukwaa ya burudani ya kimtandao duniani.

"Sina muda mrefu kwenye muziki ila nimepokewa kwa kishindo na mashabiki baada ya kuachia ngoma yangu na Tundaman. Huu ni mwanzo wa ujio wa EP yangu ambayo itatoka kabla ya mwaka huu kuisha," amesema M King Son.





# BREEDER ATAKA KUOA WAKE 200

RAPA mkali wa Kenya, Breeder LW ameweka wazi kwamba ana wapenzi wa kike wengi na ndoto yake ni kuoa wake wasiopungua 200.

Akizungumza hivi karibuni, Breeder amekanusha kuwa katika mahusiano ya kimapenzi na msanii Mandy, lakini akasema kuwa mrembo huyo ni rafiki yake kimuziki.

"Mimi unajua ni mume wa wanawake wengi, niko na mrembo katika kila eneo,mtaa na vijiji 12 vya Wakikuyu. Kusema ukweli nina ndoto ya kuoa wanawake 200." Amesema.





# H Baba mdomo utakuponza

MSANII Mkongwe wa muziki nchini, H Baba amemkabili tena nyota wa Bongo Fleva, Harmonize kwamba alikuwa akinufaika na kazi za wasanii wake wakati wenyewe wakitaabika kwa njaa.

Amesema alimshinikiza Country Boy kuondoka katika lebo ya Konde Music Worldwide ambayo inamilikiwa na Harmonize, kutokana na kutonufaika na kipaji chake.

Amesema wasanii hao walikuwa wanafanya kazi kubwa lakini wakati wa mafanikio Harmonize anajitenga na kuwahusisha wanawake kuwa ndio waliochangia.

# MTOTO WA RINGO KAFANANA NA TIN WHITE

**Na Adam Fungamwango**

LEO tunaziangalia posti za wasanii mbalimbali na watu maarufu nchini kwenye mitandao yao ya kijamii.

Mara nyingi huposti maneno na jumbe mbalimbali za kuhabarisha, kufundisha, kuelimisha na mambo ambayo wakati mwingine yamewakuta wenyewe.

**Aunt Ezekiel**

Huyu ni mlimbwende wa zamani, muigizaji na mjasiriamali, binti wa kiungo mshambuliaji wa miaka ya 1970 hadi 1980 wa klabu ya Simba Ezekiel Grayson 'Jujuman.'

Katika mtandao wake wa kijamii ameposti maneno yafuatayo.

"Siyo kila mitishamba ni dawa, mingine ni sumu."

**Gabo Zigamba**

Ni mmoja wa waigizaji bora wa kiume ambao nchi hii imebarikiwa kuwa nao, yeye ameandika maneno hata kwenye mtandao wake wa instagram.

"Wakati wa kutafuta kusudi la maisha yako , ustahimilivu ni muhimu ili kupata taswira yakinifu katika safari uendayo."

**Flora Mvungi**

Huyu ni mmoja wa wasanii wa filamu wa kike akiwa kwenye tasnia hiyo kwa miaka mingi, yeye akaamua kuachana na watu wenye dharau.

"Nampenda anayenipenda, namheshimu anayeniheshimu, kinyume na hapo hutopenda kunifahamu, maana sina unafiki. Kwangu nyekundu ni nyekundu na kijani ni kijani, sipindishi."

**Ringo**

Ringo ni mwigizaji wa michezo wa ucheshi, wenyewe wanaita 'komedi', yeye aliposti picha akiwa na mwanamke mmoja pamoja na mtoto, halafu akaandika kwenye akaunti yake.

"Nipo na familia yangu, vipi jamani mtoto kafanana na mimi au nimepigwa?" Akauliza.

Mashabiki wake walimjibu, lakini aliyetia fora ni jamaa mmoja aliyejiita Payole ambaye alikomenti.

"Mbona kafanana na Tin White?" Anayemsema amefanana na huyo mtoto naye ni msanii rafiki mkubwa wa Ringo ambaye anaigiza naye kwenye michezo mingi ya 'komedi.'

**Dula Makabila**

"Niliamini hawezi kuniumiza na hatokuja kuweza ila kama yeye kaweza basi hakuna ambaye atashindwa, maana yeye ndiye alikuwa wa mwisho kumuamini katika maisha yangu.

Moyo wangu nahisi unawaka moto, naumia sana sitaki tena mapenzi wala mahusiano sitaki sitaki sitaki sitaki tena." Anaandika maneno haya ikiwa ni miezi takriban miwili hivi tangu abwagane na mkewe Zay Lissa ndoa iliyodumu kiasi cha miezi miwili hivi.



FILAMU

# Nimekosea: Kuuza ramani ya vita

**Na Adam Fungamwango**

TUNAWEZA kusema kuwa mwanadada hapa ameuza ramani ya vita. Sasa ameshambuliwa yeye hana pa kutokea.

'Nimekosea' ni filamu inayowafundisha binadamu kutotoa siri ya kile kinachompa furaha kwenye maisha yake.

Ni kwa sababu kuna watu wengine hawataki binadamu wenzao wawe furahani. Wapo ambao wanaitafuta furaha popote pale ilipo lakini hawaipati. Unapomuelezea kuwa wewe furaha yako inapatikana wapi au kwa nani, mtu yule anaweza kuifuata na yeye aipate, haijalishi kama atakunyang'anya.

Mai na mume wake hawaishi kwa amani. Wanagombana kila siku. Sababu ni kwamba mume wa Mai hamjali mkewe, hamtunzi inavyopaswa kiasi kwamba dada wa watu hana amani na ndoa yake.

Vaa yake ya tabu, kula ya shida, kila kitu matatizo. Inafika wakati mume anamwambia apashe kiporo cha ugali wa jana ale. Hapo ndipo mke alipochoka na kumpa vipande vyake.

Akamwambia mke anahitaji nguo, chakula na matunzo, lakini yeye kila siku dela moja ambalo analisubiri likauke ndiyo avae. Mumewe akampiga kwa madai hana adabu.

Upande wa pili Mai ana shoga yake ambaye anaishi vema na mumewe Adam. Mume anamjali mkewe, akimpa kila kitu anachohitaji.

Upendo anaopewa dada huyo akawa anakwenda kuwambia shoga yake Mai.

"Yaani mwanaume huyu anavyonipenda, kila ninachotaka ananipa. Nitake nini mie mtoto wa watu. Pesa, chakula na kila kitu. Nikitaka pesa huwa ananiachia kadi ya benki nikachukue.

Pamoja na kwamba ni mtu na shoga yake, lakini kwa Mai ilikuwa kama msumari wa moto kwenye kidonda. Akawa anajiuliza, "nitampata wapi mimi mwanaume kama huyu?"

Siku moja anakwenda nyumbani kwa shoga yake, hamkuti. Anayemkuta ni mumewe. Kilichoendelea huko ni kwamba Mai alijilengesha tu kwa Adam kwa sababu ya kuvutiwa na maneno aliyokuwa akiambiwa na shoga yake. Kwa bahati mbaya wanafumaniwa. Mke wa Adam anaondoka nyumbani na Mai anapewa talaka na mumewe.

Wanawake wanamlaumu mke wa Adam wakimwambia yeye ndiye aliyesababisha ndoa yake na ya shoga yake ivunjike kwa kutoa siri yake ya ndani.





# Rihanna, ASAP wamuweka hadharani kichanga chao

MASTAA wa muziki nchini Marekani, Rihanna na mumewe ASAP Rocky wamemtambulisha rasmi mtoto wao wa pili.

Wanandoa na watoto wao wadogo walionekana kwenye picha za pamoja zilizotolewa katika mtandao wa Instagram na kumweka hadharani mtoto wao mchanga.

Kulingana na ripoti za Daily Mail, ilimtaja mtoto huyo kuwa ni Riot Rose Mayers ambaye kulingana na cheti kilichopatikana kinaonyesha alizaliwa Agosti 1, saa 7:41 katika Hospitali ya Cedar Sinai huko Los Angeles.



## Mkongwe Hugh amtaliki mkewe

MWIGIZAJI mkongwe wa Hollywood, Hugh Jackman amempa talaka mkewe Deborra-Lee baada ya kuishi katika ndoa kwa muda wa miaka 27.

Jackman ameuambia mtandao wa TMZ, amesema kwa sasa anapitia wakati mgumu wa mpito baada ya mchakato huo kukamilika.

Awali kuliibuka uvumi kwamba wawili hao wametengana licha ya kuishi kwa muda mrefu kama mume na mke.

Katika taarifa yao ya pamoja katika jarida la People Magazine, walitangaza kuachana huku wakisisitiza kuwa wanaheshimu maamuzi yao binafsi.

## Polisi waendelea kuwasaka wauaji

POLISI Jimbo la Lagos nchini Nigeria, inaendelea kuwasaka watu waliosababisha kifo cha mwanamuziki Mohbad.

Hata hivyo, idadi ya watu wanaoshinikiza polisi kuchukua hatua inaongezeka na kuwataka polisi kumkamata mwanamuziki Naira Marle, ambaye wengi wanaamini anahusika.

Timu ya askari 13 wamepewa kazi hiyo na kutakiwa kuwakamata wale wote watakaoonekana wamehusika na mauaji hayo.

Mwimbaji huyo pia alidaiwa kuomba ulinzi kutokana na kuwa na hofu.





## Toke hataki kung'ang'ania penzi

MWIGIZAJI na mwanahabari kutoka |Nigeria, Toke Makinwa amefichua kuwa angesalia kwenye ndoa yake na aliyekuwa mume wake Maje Ayida, kama angefuata tabia ya wanawake kusingizia watoto.

Amesema podikasti yake kwamba hawezi kuwahukumu wanawake ambao wanavumilia ndoa zao zenye mateso kutokana na kuwa na watoto.


"Wanawake wengi wanakaa kwenye ndoa zisizo na afya kwa sababu ya watoto. Muda mrefu unasikia wanawake wengi wakisema wanaendelea kuvumilia lakini kwangu sikufanya kwa mume tulioachana,| amesema.

## Regina ndoa yake bado imara

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Regina Daniel amesema ndoa yake na mume wake Ned Nwoko ina upendo zaidi ya kinachoonekana kwenye mitandao ya kijamii.

Regina amesisitiza kuwa tofauti na watu wanavyofikiri, ndoa yao ni thabiti na mumewe huungana naye kucheka pale anaposoma maneno ya watu mtandaoni.

"Kweli, yeye ndiye Odogwu halisi, na ndoa yetu ni tamu kuliko watu wanavyoona mtandaoni. Wakati mwingine ninapoona na mume wangu maoni ya watu wakitusema , huwa tunacheka wote wawili," amesema.



HABARI KASKAZINI

## Wavuvi washauriwa kuunganisha nguvu

**Na Hamida Kamchalla,** PANGANI

MKURUGENZI wa Kituo cha Mafunzo cha Kanda ya Ziwa – Mwanza, Prof. Juvenal Nkonoki, amevihimiza vikundi vya wavuvi na wachakataji dagaa wilayani Pangani, Tanga kudumisha umoja na ushirikiano kwani ndiyo mtaji wa maendeleo unaoweza kuwaletea mafanikio kwa haraka.

Prof. Nkonoki aliyasema hayo katika hafla ya ufunguzi wa mafunzo ya siku mbili ya kuvijengea uwezo vyama vya ushirika kwa vikundi 11 vya wavuvi na wachakataji dagaa yaliyofanyika katika kijiji cha Sakura, kata ya Kipumbwi wilayani hapa.

Mafunzo hayo yalivishirikisha vikundi hivyo vyenye wanachama 218 wakiwamo wanawake 118 na wanaume 100.

"Mkiwa katika umoja tuna imani hata tukiwajengea uwezo mtakuwa na nguvu ya kutoka pale mlipo na kwenda sehemu nyingine kwa vile mtakuwa na uwezo wa kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya uvuvi.

"Tunaamini kwa umoja wenu mafunzo haya yanakwenda kuwa chachu ya mabadiliko kwenu na mnao wawakilisha tunatarajia mafanikio makubwa kupitia mafunzo haya mliyoyapata hii leo" alisema Prof. Nkonoki.

Aidha, Prof. Nkonoki aliishukuru serikali ya Japan na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa ufadhili wao lakini pia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa uratibu wa mafunzo hayo.

Awali, mwakilishi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Meja Hassan Kheri, alisema mafunzo hayo ni moja kati ya malengo ya mradi wa kukabiliana na vitendo vya kihalifu katika bahari na maziwa makuu nchini.

Alisema Februari, mwaka huu, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alizindua mwongozo wa kukabiliana na vitendo vya uhalifu katika bahari na maziwa makuu kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo hayo.

Mratibu wa Mafunzo hayo, Dk. Bonamax Mbasa, ambaye ni Mhadhiri Mwandamizi kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini alisema mafunzo ya kuvijengea uwezo vikundi hivyo yataendelea kufanyika katika wilaya tatu ambazo shughuli zake za kiuchumi zinategemea uvuvi baharini. Alizitaja wilaya hizo kuwa ni Mafia, Pangani na Bagamoyo.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Erasto Mhina (kushoto), akisaidia kumtwisha ndoo kichwani mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika sekondari ya Chatuu, wakati wa uzinduzi wa kisima cha maji chenye thamani ya Sh. Milioni 16 kilichochimbwa na Taasisi ya Islamic Help kwa ufadhili wa watu wa Kuwait. Wengine ni Mkurugenzi wa Islamic Help, Mohasaad Mohammed (wa pili kulia), Diwani wa kata ya Kilulu, Fuard Rashid (wa tatu kulia) na (wa tatu kushoto) ni Diwani wa kata ya Mtindiro, Mustafa Hatibu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Asisitiza umuhimu kliniki VVU kwa watoto

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MRATIBU wa kudhibiti Virusi vya UKIMWI mkoani Manyara, Dk. Charles Shija, amesema watoto wenye maambukizi ya ugonjwa huo wanapaswa kuhudhuria kliniki miezi 18 ili kupatiwa dawa za kufubaza virusi na kupata ushauri wa kitaalam.

Dk. Shija alisema hayo jana wakati wa mahojiano maalumu na Nipashe juu ya kliniki za watoto chini ya miaka mitano ambao wanaishi na VVU.

Alisema watoto wa umri huo wanapata VVU nyakati tatu wakati wa ujauzito, wakati wa kujifungua na wakati wa kunyonya.

"Mtoto aliyezaliwa na VVU tunamfanyia vipimo na anapimwa kwa kipimo cha PCR ambacho kina uwezo mkubwa cha kumpima akiwa na miezi 18,"alisema Dk.Shija

Pia alisema mtoto mwenye VVU anapimwa wakati wa kuzaliwa, akiwa na wiki sita, akiwa na miezi tisa, miezi 15 na miezi 18.

Mtaalamu huyo alisema chanzo cha kuwapima mara nyingi ni kutaka kujiridhisha juu ya vipimo vilivyotangulia kwa kuwa kipimo cha kwanza au cha pili kinaweza kuwakilikosewa.

Alisema kuwa mama mwenye VVU anatakiwa anyonyeshe miezi 12 na miezi mitatu baada ya kumuachisha mtoto inabidi apimwe akiwa na miezi 15.

"Athari ambazo anaweza kuzipata mtoto akiendelea kunyonya ni taya zinakuwa zimekomaa ni rahisi kupata michubuko," alisema na kuongeza kuwa kipimo cha mwisho ambacho kinatoa uhakika ni cha miezi 18.

Kuhusu dawa wanazotumia watoto , alisema ni tofauti na watu wazima ambapo watoto dawa zao zipo kwenye mfumo wa maji, chengachenga na vidonge vinavyoyeyuka kwa wepesi.

Alivitaja vikwazo wanavyokumbana navyo kutoa huduma kwa watoto wenye VVU ni unyanyapaa, wazazi kushindwa kufuata maelekezo ya dawa na kuna wazazi ambao wanawakatia tamaa watoto wao.

Naye Mkurugenzi wa Shirika la Baraka Community Concerns Foundation, Jovin Riziki, akizungumza na Nipashe juu ya jambo hili alisema kwa mujibu wa ripoti ya mwaka 2021, watoto wa miaka sifuri hadi 14 wanaoishi na VVU ni 96,000 nchi nzima na watoto 9,400 kila mwaka wanapata maambukizi.

Riziki alisema uelewa mdogo wa wazazi na walezi unawafanya wawafiche watoto hawawaambii kuwa wana VVU na wengine wanakosa nauli za kufuata dawa za kufubaza virusi kwenye vituo vya kutolea huduma.

Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Umoja wa mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) ya mwaka 2021, watoto na vijana wanachangia asilimia 17 ya vifo vyote vinavyohusiana na UKIMWI na asilimia 21 ya maambukizi mapya ya mwaka huo ni mitindo ya muda mrefu inabaki kuwa chanya.

## Mwekezaji apewa siku saba kuondoa harufu

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limempa siku saba mwekezaji wa kiwanda cha kuzalisha funza, maarufu kama Chanzi, kudhibiti harufu kali itokanayo na taka laini zinazotumika kuzalishia bidhaa hiyo.

Kiwanda hicho huzalisha funza kwa ajili ya kutengenezea chakula cha mifugo na kwamba kuwapo kwa harufu hiyo kumekuwa kero kwa wananchi wanaoishi eneo linalozunguka sehemu hiyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria wa NEMC, Dk. Thobias Mwesiga, alitoa muda huo jana alipotembelea kiwanda hicho kilichoko mkoani Arusha.

Alimtaka mwekezaji huyo kuhakikisha anatafuta mbinu mbadala ya kuzuia harufu kusambaa na kusababisha kero kwa wakazi wanaoishi maeneo yanayozunguka kiwanda hicho.

"Tulipokea malalamiko kutoka kwa wananchi wanaoishi maeneo haya kwamba harufu kali inayosababishwa na shughuli zinazotekelezwa hapa imekuwa kero kwao, hivyo tukatumwa na Waziri anayesimamia shughuli za mazingira kuja kutembelea na kukagua shughuli hizo na tumejionea hali halisi. Sasa natoa siku saba kudhibitiwa kwa harufu hii," alisema.

Dk. Mwesiga alisema endapo muda huo utatimia na kiwanda kikawa bado kinalalamikiwa au kushindwa kutimiza sheria na kanuni za mazingira, hatua kali zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria ikiwamo kupigwa faini na kufungiwa kufanya uzalishaji.

Aliitaka halmashauri ya Jiji la Arusha kuharakisha mchakato wa upatikanaji wa eneo la mwekezaji huyo ili ahamishe kiwanda hicho na kukipeleka mbali na makazi ya binadamu.

Ofisa Mazingira wa Jiji la Arusha, Sigfrid Mbuya, alisema tayari mwekezaji huyo alishapeleka mapendekezo ya kuomba eneo la kujenga kiwanda kikubwa kwa kuwa eneo lilopo sasa limekuwa dogo.

Meneja shamba wa kiwanda hicho, Mayasa Mhina, alisema walishafanikiwa kudhibiti harufu hiyo lakini tatizo limejitokeza pindi umeme ulivyoanza kuwa wa mgawo.

Kiwanda hicho huchakata taka laini na kuzalisha funza kwa ajili ya kutengeneza chakula cha mifugo aina ya protini pamoja na mbolea.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

## MAYAULA MAYONI

# Winga wa Yanga msomi, aliyebebwa kupigia kwa Franco, hadi bendi yake

## -Yanga 2 Simba 1; alitungua mabao yote 1971

**Na Adam Fungamwango**

NDIYO ndugu zangu hebu tujadili jambo letu. Hapana shaka hanibishii mtu. Unapotaja jina la Luambo Luanzo Makiadi Franco hakuna mjadala ni jina kubwa duniani kwenye ulimwengu wa muziki wa rhumba. Vile vile unapolitaja jina la klabu ya soka la Yanga, naona hata aibu kukuuliza kama ni kubwa au siyo kubwa...

Hebu tuendelee, kuanzia zama zile nchi yetu ikiwa katika miaka 10 ya Uhuru, kwa walioshuhudia wanajua ni wangapi ndiyo waliokuwa wamekanyaga ardhi ya shule, wasiojua kusoma na kuandika kibao mtaani, hata kutapakaa shule zilizoitwa 'ngumbalu' kila mtaa na vijiji, kuwasomesha, sembuse huyo mwenye digirii ya Chuo Kikuu miaka hiyo hadhi yake inakuwaje? Ni mtu maarufu sana!

Ndugu yangu bado hatujamaliza, tuendelee! Unamkumbuka mwanamuziki Fred Mayaula Mayoni?

Naye si haba na gitaa lake akawa maarufu wa kutosha, kwa zama zake 'Luambo mdogo' fulani hivi.

Tutaenda kushoto na kulia, ni adimu sana zama hizo hadi leo hii mtu mmoja umaarufu wake kujichomeka kwenye mitaa yote hiyo.

Lakini kwa huyu mwamba, Mayaula Mayoni akayaweza akiwa na la nyongeza, Mzaire maarufu kwenye mitaa ya Dar es Salaam, kama vile mzaliwa wa Tandika au Manzese.

Yeye huyo huyo ana digirii ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tena kazama kwenye uchumi, namna ya kupanga bajeti ya mfukoni yeye ndiye mtaalam.

Ukigeuka shingo ya pili, humo humo kwenye klabu ya Wananchi ana historia ya kudhibiti namba ya winga wa kushoto wa klabu hiyo, akiweka rekodi ya kuwatungua watani zao wa jadi Simba mabao mawili katika mechi ya ligi, huku Wanambazi hao wakifutiwa chozi na bao la lililofungwa na kiungo Omari Gumbo, hiyo ikiwa ni mwaka 1971, mwanamuziki mwenzake Mbaraka Mwinshehe Mwaruka mwaka huo akitamba na miaka 10 ya Uhuru.

Katika hilo hilo lililompaisha sana Mbaraka-muziki, naye Mayaula si haba, akavua jezi za mpira wa miguu, akaweka digrii yake pembeni, akabaki na sanaa tu iliyompagawisha Franco na kumjuisha kwenye safi yake ya wanamuziki wake bora.



Mayaula akiwa jukwaani na gitaa lake la rhythm akifanya kazi ya muziki baada ya kutundika daluga.

Hapo nikunong'oneze jambo...Yaani zamani kulikuwa na mambo, we acha tu! Kwa kifupi Franco akikuchagua kwenye kikosi chake cha TP OK Jazz kwa maana yake kikosi kilichokamilika, ujue nawe ni pedeshee wa muziki haswa. Sasa Mayaula alikuwa hivyo.

Kutoka darasani, uwanjani mpaka jukwaani, hiyo ndiyo digrii ya Congo DR. Kama haitoshi, mbele ya safari Mayaula akanogewa kimuziki na kimaisha, hata kisomi kwenye fani yake ya uchumi, akazama na kuanzisha bendi yake...aliyotamba nayo kwa muda mrefu, pasipo kusahau Dar es Salaam yake, tangu ujana hadi uzeeni, kila akipakumbuka mara kaonekana Kinondoni, mara Magomeni, mwenyeji wa kutupwa Kinondoni Mkwajuni, hata Sinza mji uliokuwa baadaye wakati yeye alishaondoka hakukosekana.

Sasa nikupe la kuondoka nyumbani, au kwenda kujadili soka kwenye kahawa; Huyu ndiye mchezaji wa aliyepanda mbegu ya urafiki wa klabu ya Yanga na wachezaji wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, historia leo ikidumu zaidi ya miaka 50. Upo hapo?

**ALIVYOJIUNGA NA YANGA**

Alizaliwa nchini Zaire mwaka 1946 (sasa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo) na akasoma shule ya msingi, akamaliza elimu yake kwenye Chuo cha Kisantu miaka ya 1960.

Wakati huo wote akiwa bado mdogo alikuwa na kipaji cha utunzi na kuimba muziki wa dansi, pia fundi wa kandanda akicheza winga wa kushoto.

Ustadi wake kwenye soka ulimfanya kusajiliwa na AS Vita Club mwaka 1968 na muda mfupi tu baadaye alichaguliwa kwenye kikosi cha timu ya taifa ya nchi yake Zaire (DRC).

Historia inaeleza kuwa baba yake alikuwa mwanadiplomasia, hivyo alitolewa nchini kwao na kuletwa nchini Tanzania kikazi.

Hapo ndipo Mayaula alipomfuata baba yake nchini na akajiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimasomo.

Pamoja na hayo akili yake ilikuwa katika soka, hivyo alisaka timu ya kuichezea. Duru zinasema alikwenda kwanza kwenye klabu ya Simba na walionekana kumdharau licha ya baadhi ya wachezaji kushinikiza achukuliwe kwa sababu anamfahamu alikuwa mchezaji wa AS Vita, lakini hakufanikiwa.

Akaamua kwenda Jangwani ambapo alipokelewa na kuwa mchezaji wa Yanga, ndipo alipolipa kisasi cha kukataliwa kwenye klabu ya Simba kwa kuwafunga mabao mawili mguuni mwake timu hizo zilipokutana kwenye ligi, Yanga ikishinda mabao 2-1.

Alidumu kwa msimu mmoja tu, akaelekea nchini Ubelgiji kujiendeleza kimasomo pamoja kucheza soka kwenye klabu za Racing Club de Charleroi na Racing Club de Jette' ya Brussels.

Baadaye alitimkia kwenye klabu ya FC Fribourg ya Switzerland na huko ndiko alikoanza kujifunza rasmi gita katika bendi ya Wakongomani nchini humo ikiitwa Orchestra Africana, pamoja na utunzi na kuomba akaongeza ujuzi wa kupiga gita la kati rhythm.

Kumbuka mpaka kipindi hicho alikuwa akiitwa kwenye kikosi cha timu ya taifa na mara ya mwisho ilikuwa ni 1974.

**ACHUKULIWA NA FRANCO**

Aliporejea nchini Zaire aliamua kujipumzisha na masuala la soka na kujikita kwenye muziki.

Kwa sababu tangu zamani alikuwa na kipaji hicho haikuchukua hata muda kuonekana na gwiji Franco akamchukua kwenye bendi yake ya TP OK Jazz.

Naye kwa kuonyesha kuwa hawajakosea alitunga wimbo uliotetemesha Afrika nzima katikati ya mwaka 1975, 'Cherie Bondowe.'

Ni wimbo uliovuma na kupendwa hata na wamamuziki wa bendi zote nchini humo, achilia mbali mashabiki wa rhumba Afrika nzima.

Katika kuonyesha kuwa hakubahatisha alitunga wimbo na kumpa mwimbaji wa kike Mpongo Love ambao umeendelea kupendwa hadi leo hii 'Ndaya.'

Wengi wanadhani mtunzi ni Mpongo Love, lakini ukweli ni wimbo wa Mayaula Mayoni.

Baada ya kuwa maarufu sasa kwenye muziki na kujiona anaweza kusimama mwenyewe aliamua kuanzisha bendi yake ambapo alianza kufyatua vibao mbalimbali kiasi cha kuchaguliwa kuwa mtunzi bora wa DRC mwaka 1978.

Wabongo wengi wanaufahamu wimbo wa 'Mboungue' wenyewe wanauita 'Mbongwe', alioutunga mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Zingine ni 'Nabali Misele', 'Kotikate', 'Bondowe no 2', 'Ousmane Bakayoko', na 'Nasi Nabali' ambao alimpa mwanadada Tshala Muana kuuimba.

**KIFO CHAKE**

Mayaula aliamua kuhamia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi ubalozi wa Congo kama baba yake. Wakazi wengi wa Magomeni jijini Dar es Salaam watamkumbuka Mayaula, ambaye katika kipindi hicho akifanya kazi ubalozini, alikuwa akiishi maeneo hayo.

Alianza kuugua akiwa hapa hapa nchini, akaamua kurudi kwao Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Hali ya afya yake ilizidi kuwa mbaya mwaka 2005 serikali ya kwao ilimpeleka nchini Ubelgiji kwa matibabu zaidi.

Hata hivyo juhudi hizo hazikuzaa matunda kwa Mayaula akafariki dunia katika jiji hilo la Brussels nchini Ubelgiji Mei 26, 2010 akiwa na umri wa miaka 64. Huo ukawa mwisho wa mwanamuziki na mwanasoka msomi.



Mayaula Mayoni (kushoto aliyezungushiwa duara) akiwa na kikosi cha timu ya taifa ya Zaire (DRC) mwaka 1974.

# Wanafunzi 90 wala keki yenye bangi, wachanganyikiwa wakiwa darasani

**CAPE TOWN,** AFRIKA KUSINI

WATOTO 90 wa shule ya msingi nchini Afrika Kusini walipelekwa hospitalini baada ya kula keki zinazodhaniwa kutiwa dawa za kulevya aina ya bangi.

Maofisa walisema wanafunzi hao walinunua keki hizo kutoka kwa mchuuzi mmoja wa barabarani walipokuwa wakielekea Shule ya Msingi ya Pulamadibogo, kaskazini-magharibi mwa Pretoria.

Walisema baada ya kula walipata hali ya kichefuchefu, maumivu ya tumbo na kutapika na wanafunzi watatu wasichana hali yao nzi nzuri wamelazwa hospitalini.

Tayari watu wawili wamekamatwa na wanakabiliwa na mashtaka ya kujaribu kuua.

Washukiwa hao, wenye umri wa miaka 21 na 19, walifikishwa jana katika Mahakama ya Soshanguve kwa ajili ya kusomewa mashtaka yanayowakabili.

Idara ya elimu ya mkoa wa Gauteng ilisema walimu waliita gari la wagonjwa baada ya kuona wanafunzi hao wamebadilika kitabia na kufanya mambo ya ajabu walipokuwa darasani.

Ilisema tukio hilo limesababisha masikitiko kwa wazazi ambao walikuwa na wasiwasi kuhusu usalama wa watoto wao.

Polisi ambao wanaendesha uchunguzi ili kuthibitisha kama bangi ilitumika kuchanganywa na keki hiyo, walisema zaidi ya wanafunzi 90 walikula keki hizo na wote walipata tatizo la maumivu makali.

Watoto 97 ambao walikimbizwa katika vituo mbalimbali vya matibabu afya jirani na shule hiyo waliruhusiwa kwenda nyumbani.

"Wanafunzi watatu wasichana pekee ndio wamesalia hospitalini, na bado wanapokea matibabu muhimu ili kurudi katika hali zao za kawaida," ilisema.

**BBC**

# Armenia yailaumu Arzerbaijan kwa maujia

**NEW YORK,** MAREKANI

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Armenia, Ararat Mirzoyan amesema mashambulizi ya ukatili yaliyofanywa na Arzerbaijan dhidi ya Waarmenia walioko katika jimbo la Nagorno-Karabkh ni sawa na mauaji ya kimbari.

Mirzoyan aliliambia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwamba zaidi ya watu 200 walikufa kwenye mashambulizi yaliyofanyika kwa wiki hii pekee na watu wengine 400 wamejeruhiwa.

Alisema watu walioathirika na mapigano hayo ni wanawake na watoto.

Waziri huyo alilitaka Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lichukue hatua.

Nchi hizo mbili za Armenia na Azerbeijan zamani zilikuwa nchi ziliozo katika umoja wa kisovieti zimekuwa zikipigania jimbo la Nagorno-Karabakh kwa miongo kadhaa.

Umoja wa Mataifa umetoa wito kwa pande zote zinazohusika katika mzozo huo zifanye mazungumzo ya kutafuta amani.

**DW**



Fundi wa mavazi akimaliza kazi kwa ajili ya wateja wake katika mji wa Niamey, nchini Niger jana, **PICHA: AFP**

# Kanali Doumbouya akemea Ulaya kugeuza Waafrika kama watoto

**NEWYORK,** MAREKANI

KIONGOZI wa kijeshi nchini Guinea, Kanali Mamady Doumbouya, amezikaripia nchi za Magharibi kutaka mtindo wao wa kidemokrasia kufuatwa barani Afrika, akisema waache kuwafanya kama watoto.

Kanali Doumbouya, aliliambia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mjini New York kwamba bara hilo lilikuwa likiteseka kutokana na mfano wa utawala uliotwikwa juu yao.

Alisema mifumo hiyo haiendani na hali halisi ya Afrika. "Wakati umewadia muache kutusomea na kutufanya kama watoto," alisema.

Kiongozi huyo wa kijeshi alichukua mamlaka baada ya mapinduzi ya 2021, na kumuondoa madarakani Rais Alpha Conde. Alitetea hatua yake ya kuingia madarakani ni kuokoa nchi yake kutokana na machafuko kamili. Mapinduzi hayo yalipokelewa kwa furaha na raia wa Guinea wakielezea kufarijika kuondolewa kwa Rais Conde. Nchi hiyo iliondolewa katika jumuiya ya nchi za Afrika Magharibi (Ecowas), baada ya jeshi kuchukua hatamu, huku viongozi wa kikanda wakishinikiza kurejeshwa kwa utawala wa kiraia.

Mwaka jana, Kanali Doumbouya alitoa ratiba ya mpito kwa serikali iliyochaguliwa baada ya mazungumzo na Ecowas, lakini hakuna hatua iliyopigwa katika kuandaa uchaguzi mkuu.

Guinea ni miongoni mwa nchi kadhaa za Afrika magharibi na kati ambazo zimeshuhudia mapinduzi katika miaka ya hivi karibuni zikiwemo Mali, Burkina Faso, Niger na Gabon.

**BBC**

# Jenerali Burhan aonya vita itasambaa

**NEW YORK,** MAREKANI

KIONGOZI wa jeshi la Sudan ameonya kwamba vita vya nchi yake vinavyoendelea vinaweza kusambaa katika mataifa jirani ya Afrika.

Katika hotuba yake katika Baraza la Umoja wa Mataifa, Jenerali Abdel Fattah al-Burhan pia aliitaka jumuiya ya kimataifa kuwatambua wapinzani wake, kundi la Rapid Support Forces (RSF), kama kundi la kigaidi.

Wakati huo huo, kiongozi wa RSF Jenerali Hamdan Dagalo alisema yuko tayari kwa usitishaji mapigano.

Mnamo 2021, majenerali hao wawili walifanya mapinduzi, lakini katika miezi ya hivi karibuni mzozo wa kuwania madaraka kati yao umesababisha wafuasi wao kuchukua silaha na kukabiliana. Akizungumza kwenye mkusanyiko huo, Jenerali Burhan alisema chama chake kiko tayari kwa mazungumzo ya amani, na alitaka kukomesha vita na kupunguza mateso ya watu.

Hata hivyo, alisema wito wake wa maridhiano RSF wamekataa.

Katika ujumbe wake adimu wa video kwa Umoja wa Mataifa, mpinzani wake, Jenerali Dagalo anayejulikana pia kama Hemedti, alisema yuko tayari kushiriki mazungumzo.

**BBC**

# Ruto: Umoja wa Mataifa hakuna usawa

**NEW YORK,** MAREKANI

RAIS wa Kenya William Ruto, amelishambulia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa kulitaja kuwa ni jukwaa lisilofanya kazi vizuri na lisilo na uwakilishi.

Ruto alisema hayo alipoihutubia hadhara kuu ya Umoja wa Mataifa juzi mjini New York.

Alitoa wito kwa Umoja wa Mataifa kubadili mwelekeo kutokana na hali halisi ya sasa. "Ikiwa uthibitisho wowote uliwahi kuhitajika kwamba Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa halifanyi kazi vizuri, halina demokrasia, halijumuishi watu wote, haliwakilishi na kwa hivyo haliwezi kuleta maendeleo ya maana katika ulimwengu wetu kama ilivyo sasa, basi kutoadhibiwa kulikoenea kwa baadhi ya watendaji katika jukwaa la kimataifa kunatoa jibu kwa hilo," alisema rais Ruto.

Ruto pia aliangazia nchi ya Haiti na akauhimiza Umoja wa Mataifa kutoa utaratibu wa dharula ya kupeleka vikosi vya kiusalama kama sehemu ya mpango mpana wa kukabili changamoto ndani ya nchi hiyo.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SALMA SHABANI RASHID** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI SEKONDARI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NO. **S.1361-0118-2011** CHA SHULE YA SEKONDARI SAMORA MACHEL KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI NECTA.
YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KWA RB NAMBA **PHQ/DAR/KIN/16146/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JANE MLAY SIRIWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T972AQJ** aina ya Suzuki ESCUDO. Chassis No. **TDOIW150019**, Engine No. **G16A356269.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/250646/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GOODLUCK GEORGE KATEMBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 640 CCQ** aina ya **TOYOTA RAV 4.** Chassis No. **SXA110170416.** Engine **No. 3S2417914.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **IRI/RB/474/2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE
AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 29 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE KILEN MUHOGA CHEDEGO
AND
IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION
BY HAMIDA MOHAMEDI KWEZATUHU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 19th day of OCTOBER, 2023.

**Dated at Korogwe this 22nd Day of SEPTEMBER, 2023**

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

**SUMMONS TO APPEAR ( order V,R(1)of CPC(Substituted Service)**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
ARUSHA SUB-REGISTRY
AT ARUSHA**

**CIVIL CASE NO.230 OF 2023**

**CRDB BANK PLC............................................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**GODWIN LUDWING MAIMU.......................1ST DEFENDANT**

**TWIN LAND HOLDING LIMITED............. 2ND DEFENDANT**

**TO:TWIN LAND HOLDING LIMITED**

**WHEREAS:** The above named PLAINTIFF have instituted a SUMMARY PLAINT against you, you hereby summoned to appear in this cout in person or by an Advocate or Agent duly authorised on 25th day of September 2023 at 09:30am before Hon.D.C.Kamuzora ,Judge to answer the claim,and you are directed to produce on that day all the document upon which you intend to rely in support of your appearance on that day before mentioned the plaint will be heard and determined in your absence.
GIVEN under my hand and seal of the court this 31st day of August 2023

DEPUTY REGISTRAR
ARUSHA

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TANGA**

**Kituo cha MJINI – TANGA Mkoa wa TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 168/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MICHAEL SINDUKA SITA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA STELLA MICHAEL ISSITA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 06 Mwezi wa 10 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 22 Mwezi wa 09 Mwaka 2023.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MJINI TANGA

**FOMU MADAI - 3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**

**Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya Geita**

**Kituo cha Nyankumbu Mkoani Geita**

**Shauri la Madai ya Ndoa namba 37 la mwaka 2023**

**Jina la Mdai............................................................Marry Mussa**

**Jina la Mdaiwa......................................................Sospeter Mtani**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za Kuratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa; SOSPETER MTANI**

**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba MADAI YA TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 5 Mwezi wa 10 Mwaka 2023 saa 2:00 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe **21 Mwezi 09 Mwaka 2023.**

HAKIMU
RESIDENT MAGISTRATE
GEITA.

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0745 700 710.

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-27

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Walitoka na kutembea kwa miguu. Nancy alidhani wanakwenda kupanda basi. Walipofika maeneo ya Mwenge sokoni ndipo aligundua kuwa jamaa ana gari.

"Enhee unaishi wapi nikupeleke bibie."

"Boko."

Gari ilitafuna lami mpaka Boko.

"Nashukuru nishushe hapa hapa nimefika."

"Sasa kama tulivyoahidiana, Jumamosi ijayo nitafika hapa hapa kukuchukua sawa?"

"Saa ngapi?"

"Saa mbili usiku. Tunaweza kupitisha usiku mmoja na wewe? Yaani usirudi nyumbani?"

"Sawa wewe tu."

Nancy alijiona ni mwanamke mwenye bahati zake.

"Mwanamke niliyeombewa dua na wazazi wangu. Niliyetolewa mikosi. Niliyeoga maji ya bahari. Katoka bwana wa maana, kaingia bwana wa sheria yake." Akajitapa kimoyomoyo.

********************************

Kila mmoja alikuwa na hamu na mwenzake. Nancy alikuwa na hamu kukutana na Eddy kwa sababu baada ya kuachana na Charton hakuwa na mwanaume yeyote wa maana hadi alipojaaliwa kumpata bwana huyo kwa bahati tu.

Kuwa na bwana aliyeonekana yupo vizuri kiuchumi kama alivyokuwa Charton pia ilimfurahisha kwa sababu si jambo rahisi kiasi hicho. Akaona kabisa kuwa Mungu amemuumba na kumuachia kitu kinaitwa bahati, hivyo hatoadhirika.


Ilikuwa ni tofauti kidogo na Eddy. Lengo lake ni kufanya upelelezi. Moja ya mambo ambayo wapelelezi wanatakiwa kufanya ili kujiweka karibu na adui au kukusanya ushahidi na kukubali kuwa na mpenzi mwenye faida.

Ni yule ambaye atakupa ushahidi, nyaraka au kukufikisha mbele ya mtu unayemhitaji au anayehitajika.

"Karibu Nancy" Eddy alimkaribisha kwenye hoteli moja kubwa ya kifahari katikati ya jiji.

Aliingia kwenye chumba kikubwa cha fahari ambacho kina kila kitu.

Chumba kikubwa kilichokuwa na kitanda kikubwa cha kifahari, mashuka yaliyotandiwa kwa nakshi, pazia za gharama, friji lililojaa matunda, soda, maji na pombe, ukutani kukiwa na televisheni.




**"Umeanza hivyo, unajua mimi sipendi mtu aniuliza habari za mbwa yule."**

Nancy mwenyewe alikiri kuwa katika usichana wake wote hajawahi kuingia au kupelekwa sehemu kama hiyo na mwanaume yeyote.

Baada ya stori mbili tatu za hapa na pale waliulizana kama wale kabisa, lakini kila mtu alionekana ana hamu na mwenzake badala ya kula.

Mazungumzo yaliishia kwa Eddy kuanza kushika mkono wa Nancy aliyeonekana kama hataki, lakini anataka.

Vidole vya Eddy vilianza ziara kwenye mwili mororo wa mwanamama na mwenyewe ambaye awali alionekana anaweza kumdhibiti kwa kumzuia, aliacha ziara hiyo iendelee maeneo mbalimbali mwilini huku akiwa amefumba macho kwa hisia kali na kutetemeka kwa mbali.

Wote sasa walishindwa kujizua. Wakakumbatiana na kila mmoja alianza kuhisi kama wanapaa angali, wanakwenda sehemu isiyojulikana.

Hakuna aliyejielewa tena kama yupo kwenye hoteli ya Panama iliyopo maeneo ya Kisutu, Dar es Salaam.

Akili zilipowarudia kila mmoja alionekana kuhema zaidi ya mwenzake. Waliinuka kivivuvivu na kuelekea bafuni kuoga.

Waliporejea walikaa kwenye sofa la watu wawili lililokuwa pembeni mwa kitanda na meza ndogo wakaanza kula.

Eddy alirudia na akili mara nyingi zaidi kuliko Nancy. Wakati wanadada akiwaza kilichotokea akiwa na bwana yake mpya, mwanaume alifikiria jinsi gani anaweza kupata habari za Charton.

"Hebu mpenzi nieleze mligombana nini na Charton?"

"Umeanza hivyo, unajua mimi sipendi mtu aniuliza habari za mbwa yule."

"Sivyo hivyo mpenzi nataka kuwa na uhakiwa wewe ni wangu. Nahitaji kujua kama mlichoachania hakitafanya mrudiane tena."

"Sina haja ya kuwa na mwanaume kama yule muuaji."

"Muuaji?" Akauliza Eddy akijifanya anashangaa. Lakini hili pia alishawahi kumsikia akisema siku ile alipojifanya Chimozi.

"Yaani mimi naogopa tu ana pesa na baadhi ya askari siyo waaminifu ningekwenda kumchoma kuwa amesababisha kifo cha mkewe Tessy."

"Amesababisha au amemuua?" Akauliza kimtego.

"Amemuua."

"Kwa sababu gani?"

"Mimi nakwambia wewe Denis kwa sababu wewe umeshakuwa mpenzi wangu, iwe siri vinginevyo utakamatwa." Denis ni jina la Eddy ambalo alimdanganya Nancy na pia hakutaka kumpeleka nyumbani kwake maeneo ya Victoria kwa sababu za usalama.

"Sababu ni Rukia. Rukia ni mpenzi wake ambaye kwa sasa yupo naye."

"Kwa hiyo amekuacha wewe kamchukua Rukia si ndiyo."

"Ndiyo"

"Basi hana akili." Akasema Eddy na kusababisha Nancy aangue kicheko, halafu akauliza, "kwa nini?"

"Anawezaje kumuacha mtoto mzuri kama wewe?"

Alipomaliza kucheka Nancy kaendelea huku akitabasamu.

"Kamchukua Rukia kwa sababu amemsaidia kwenye mauaji ya mkewe."

"Hebu nyoosha basi mpenzi, mbona unaongea kama zile taarabu za zamani za mafumbo?"

Nancy akaangua tena kicheko, "jamani wewe mtu, sijakupatia mwezako."

"Na mimi sitaki unipatie mwenzangu, nataka niwe mimi tu."

"Unanichekesha bwana, mimi nataka kukwambia wewe unaleta utani."

"Haya tuendelee mama."

"Mpenzi nikwambie kitu, kuna wanaume wabaya sana duniani. Mimi nilikuwa ni mpenzi wa Charton, yaani mchepuko wake, huku yeye ana mke ambaye ndiyo huyo marehemu Tessy.

Kilichotokea ni kwamba Rukia alimpelekea Charton picha moja ambayo ndiyo imeleta maafa yote hayo.

Hiyo picha ya mnato, ni ya mwanaume mmoja amepiga na Tessy. Baada ya hapo ndipo Charton alipoanza kumuwinda mkewe taratibu na kumuua baadaye bila ya kushtukiwa na mtu yoyote. Hadi leo yupo mtaani Nadhani alijipanga. Huyo mwanaume naye alisakwa nakwambia kama mhaini lakini hakupatikana.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# FAINALI YA NCBA GOFU SERIES 2023 YAKARIBIA

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya gofu maalumu yajulikanayo kwa jina la NCBA Golf Series yamepangwa kufanyika Septemba 30, mwaka huu kwenye viwanja vya Gymkhana jijini, Dar es Salaam imeelezwa.

Lengo la mashindano hayo ni kupata wawakilishi watatu wa Tanzania watakaokwenda kuwakilisha taifa katika michuano ya Afrika Mashariki itakayofanyika baadaye mwaka huu huko Nairobi, Kenya.

Taarifa kutoka kwa waandaaji zinasema mashindano hayo yanatarajiwa kuwa na mvuto na yatakusanya vipaji vya juu vya nyota wa mchezo huo nchini.

**"Mashindano haya hayatoi tu fursa kwa nyota wa gofu nchini kuonyesha uwezo wao, bali pia kuacha majina yao katika vitabu vya historia ya mchezo huu," walisema waandaaji.**

Taarifa iliongeza wachezaji watashindana katika vipengele vitatu ambapo mshindi wa jumla, mshindi wa jumla kwa wanaume na mshindi wa jumla kwa wanawake.

Washindi watatu wa jumla wa mashindano haya wataondoka na kitita cha shilingi za Kenya 100,000.

Iliongeza gharama za safari za wawakilishi wa Tanzania zitalipiwa Benki ya NCBA na lengo lao ni kuhakikisha wachezaji wanaifurahia safari yao na kuleta heshima kwa taifa lao.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NCBA, Claver Serumaga, alisema benki yao inafuraha kuwa sehemu ya mashindano hayo ambayo yanaunga mkono juhudi za kuinua michezo Tanzania.

"Tunafuraha kubwa kuona vipaji na shauku ya wachezaji wa gofu nchini Tanzania. Tukio hili siyo tu linaonyesha ujuzi wao lakini pia linawapa jukwaa la kuwakilisha nchi yetu kimataifa. Tunatarajia mashindano mazuri na tunawatakia kila la heri washiriki wote," alisema Serumaga.

Aliongeza tayari wachezaji kutoka vilabu mbalimbali vya gofu nchini wameanza kujisajili ili kushiriki katika mashindano hayo na wanasisitiza washiriki kujiandikisha mapema.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NCBA, Claver Serumaga akionyesha uwezo wake wa kucheza gofu ikiwa ni maandalizi ya mashindano ya NCBA Golf Series 2023 yatakayofanyika Septemba 30, mwaka huu jijini, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ferry: Kiwango Azam safi

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Azam Fc, Bruno Ferry amesema amefurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Singida Fountain Gate uliochezwa Dar es Salaam na kumalizika kwa wenyeji kupata ushindi wa mabao 2-1.

Ferry alisema licha ya kucheza vizuri lakini bado wana kazi ya kufanya katika safu ya ulinzi ambayo inatakiwa kuongeza umakini na kuruhusu mabao.

Kocha huyo alisema mechi hiyo ilikuwa na ushindani mkubwa kwa sababu ya ubora wa wapinzani wao ikiwamo safu yao ya ulinzi, ushambuliaji na viungo.

"Haikuwa mechi rahisi, nina furaha kubwa kuona wachezaji wamecheza vizuri licha ya kuwapo na changamoto ikiwamo safu ya ulinzi kuruhusu bao wakati tunaongoza bao 1-0," alisema kocha huyo.

Naye kocha Msaidizi wa Singida Fountain Gate FC, Thambo Senong, alisema walishindwa kuwa makini katika mchezo huo baada ya kufanya makosa na kuadhibiwa.

Hata hivyo aliwapongeza wapinzani wake kwa kupambana na hatimaye kupata goli la jioni ambalo liliwapa ushindi katika mechi hiyo.

"Haukuwa mchezo rahisi, tunarejea kwenye uwanja wa mazoezi kufanyia kazi mapungufu yetu, tunaamini tutakuwa vizuri katika mechi iliyoko mbele yetu ya mashindano ya kimataifa dhidi ya Future FC, " alisema Thambo.




## Dabi ya Mbeya sasa kupigwa Mtwara leo

**Na Adam Fungamwango**

TIMU mbili za jijini Mbeya zenye upinzani mkali, Mbeya City na Mbeya Kwanza zinatarajia kukutana nje ya mkoa huo katika mechi ya Ligi ya NBC Championship itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Mtwara.

Hii itakuwa ni mara ya kwanza kwenye historia ya 'dabi' hiyo kuchezwa nje ya Mbeya kwa sababu Mbeya Kwanza inautumia uwanja wa Nangwanda.

Si mara ya kwanza kwa timu hiyo kucheza nje ya maskani yake jijini Mbeya kwani hata ilipokuwa inacheza Ligi Kuu Tanzania Bara kuna wakati iliukimbia Uwanja wa Sokoine na kupeleka mechi zake kwenye Uwanja wa Majimaji, Songea.

Mbeya City yenye pointi sita itashuka dimbani ikiwa kileleni Mbeya Kwanza ikiwa katika nafasi ya nne baada ya kujikusanyia pointi nne.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni wabuguruza mkia Cosmopolitan watakuwa wenyeji wa TMA kutoka Arusha na Maafande wa Ruvu Shooting watawaalika Ken Gold kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro.

## TAFF kutambulisha timu ya wanawake

**Na Shufaa Lyimo**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu kwa watu wenye ulemavu Tanzania (TAFF), limesema lipo mbioni kuanzisha timu ya wanawake ili iweze kushiriki katika mashindano mbalimbali watakayoalikwa, imeelezwa.

Akizungumza jijini jana, Rais wa TAFF, Vicent Kaduma alisema mchakato wa kuanzisha timu hiyo unaendelea vyema na watahakikisha wanakuwa na kikosi bora cha wanawake.

"Tupo kwenye mchakato wa kuanzisha timu ya wanawake kwa upande wa watu wenye ulemavu, ninaamini muda si mrefu timu hiyo itakuwa tayari kutokana na juhudi tunazoendelea kuzifanya," alisema Kaduma.

Aliongeza uongozi wake unaahidi kushirikiana vyema na Baraza la Michezo la Taifa ( BMT) katika kuhakikisha wanatekeleza vizuri majukumu waliyopewa.

Alitaja baadhi ya majukumu waliyopewa ni kuratibu usajili wa wanachama, mchakato wa uchaguzi mkuu, kuratibu marekebisho ya katiba na kuunda kamati ndogo ndogo zitakazowawezesha kukamilika kwa maagizo hayo.

## ZISIKUPITE

**THURAM AGOMBEWA ULAYA**

KLABU ya Juventus imeungana na Liverpool, Paris St-Germain, Bayern Munich na Tottenham Hotspur katika mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa, Khephren Thuram mwenye umri wa miaka 22 kutoka Nice. (*90 Min*)

**EZE, PALACE KUTETA**

KLABU ya Crystal Palace inatarajiwa kuanzisha mazungumzo ya awali kuhusu mkataba mpya na winga wa England, Eberechi Eze mwenye umri wa miaka 25, ambaye mkataba wake wa sasa utaendelea hadi mwaka 2025. (*Athletic*)

**UNITED KUMUUZA SANCHO**

MANCHESTER United iko tayari kumuuza winga wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, ambaye walimnunua kwa pauni milioni 73 kutoka Borussia Dortmund, kwa bei iliyopunguzwa Januari. (*Star*)

**SON, SPURS KIMEELEWEKA**

KLABU ya Tottenham Hotspur inatazamiwa kutekeleza kipengele cha chaguo katika mkataba wa mshambuliaji wa Korea Kusini, Son Heung-min mwenye umri wa miaka 31, ambao utaongeza mkataba wake kwa mwaka zaidi na hivyo kumalizika ifikapo 2026. (*Telegraph*)

**MADRID, BAYERN VITANI**

KLABU ya Bayern Munich itachuana na Real Madrid kumsajili nahodha wa Chelsea na beki wa pembeni wa Timu ya Taifa ya England, Reece James hapo mwakani. (*Fichajes*)

**CHOLOBAH KUTUA BAYERN**

MLINZI wa Chelsea, Trevoh Chalobah anatazamiwa kuondoka katika klabu hiyo ifikapo Januari, huku beki huyo mwenye umri wa miaka 24 akitaka kuhamia Bayern Munich baada ya kuikataa Nottingham Forest. (*Fabrizio Romano*)

**XAVI KUBAKIA BARCA**

KOCHA wa Barcelona Xavi amekubali kuongeza mkataba wa mwaka mmoja hadi 2025 katika mkataba ambao una chaguo la kuongezwa kwa miezi 12 mingine. (*ESPN*)

**NUSA AGEUKA LULU EPL**

ARSENAL, Chelsea na Manchester United zinavutiwa na winga wa Norway na Club Bruges, Antonio Nusa, mwenye umri wa miaka 18 na thamani yake ni karibu pauni milioni 30. (*Express*)

**NAGELSMANN MAMBO SAFI**

KOCHA wa zamani wa Bayern Munich, Julian Nagelsmann mwenye umri wa miaka 36, anakaribia kufikia makubaliano ya kuwa kocha mpya wa Ujerumani. (*Fabrizio Romano*)

**ALCANTARA, MATIP KIKAONI**

KLABU ya Liverpool iko tayari kuwasiliana na wawakilishi wa kiungo wa kati wa Hispania, Thiago Alcantara mwenye umri wa miaka 32 na beki wa Cameroon, Joel Matip (32) kwa kujadili mikataba mipya. (*Caught offside*)

**LUKAKU AJIPANGA UPYA**

MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji, Romelu Lukaku alitengana na wawakilishi wa Roc Nation muda mfupi baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 kuhamia AS Roma kwa mkopo kutoka Chelsea msimu huu. (*Telegraph*)

**ANTONIO ATAJWA SOKONI**

TIMU kadhaa za Ligi Kuu England zikiwamo Wolves, Everton na Nottingham Forest ziko tayari kumnunua, Michail Antonio ikiwa mshambuliaji huyo wa Jamaica mwenye umri wa miaka 33, atashindwa kuafikiana na West Ham kwa mkataba mpya. (*Football Insider*)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# FELIX: NILISHINDWA FALSAFA ZA ATLETICO

**●●● Mshambuliaji huyo alilazimika kukatwa mshahara ili kutua...**

**BARCELONA,** Hispania

JOAO Félix amesema hakuwahi kuzoea maisha ya Atletico Madrid au mipango ya Kocha, Diego Simeone baada ya kuanza vyema soka lake na Barcelona.

Félix mwenye umri wa miaka 23, amefunga mara tatu katika mechi zake mbili za kwanza alizoanza Barca baada ya kujiunga na klabu hiyo kwa mkopo wa msimu mzima akitokea Atletico mapema mwezi huu.

**Mshambuliaji huyo wa Ureno alisasajiliwa Atletico akitokea Benfica kwa euro milioni 126 mwaka 2019, lakini hakuwahi kufikia matarajio katika misimu minne aliyocheza chini ya Simeone.**

"Mambo yanapoenda vibaya katika soka kwa mtu, lazima ufanye mabadiliko," alisema Félix katika mahojiano na Mundo Deportivo.

"Nilifanya hivyo kabla ya kwenda Chelsea (kwa mkopo katika kipindi cha pili msimu uliopita) na sasa kuja Barcelona kwa sababu sikuwa naendelea vizuri kule Atletico.

"Sikukubaliana na mawazo ya klabu au kocha, lakini kila mara nilijaribu kufanya kitu bora niwezavyo. Nimekuwa na nyakati nzuri huko pia."

Félix alikataa kwenda Saudi Arabia akisubiri nia ya Barca, na hatimaye makubaliano yalifikiwa siku ya mwisho ya dirisha la uhamisho wa majira ya joto.

Ili kukamilisha usajili huo wa mkopo huo, ilibidi Felix akubali kukatwa kiasi kikubwa cha mshahara wake iliyotokana na matatizo ya kifedha ya Barca.

"Ni kweli niliacha sehemu kubwa ya mshahara wangu, lakini nilihitaji mabadiliko," aliongeza.

"Nilihitaji kufika mahali ambapo naweza kucheza mtindo wangu wa soka na nimekuwa nikisema kila mara nadhani hapa ni mahali pazuri.

"Mambo yanakwenda vizuri, sikutarajia kuanza vizuri, na ilikuwa ni juhudi nilizohitaji kufanya ili kupata furaha ya kucheza soka tena."

Félix alifunga bao lake la kwanza dhidi ya Real Betis wikendi iliyopita na kufuatiwa na mabao mawili katika ushindi wa 5-0 dhidi ya Royal Antwerp kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumanne iliyopita.

Matokeo hayo yalimsukuma Kocha wa Barca, Xavi Hernandez kudai timu yake inacheza soka lao bora tangu achukue mikoba yake mwaka 2021.

Kusajiliwa kwa Félix kumechangia kuimarika kwa kiwango hicho, lakini mchezaji mwingine mpya aliyesajiliwa, João Cancelo, pia amekuwa na jukumu muhimu tangu ajiunge naye kwa mkopo akitokea Manchester City.

"Kwa upande wa ubora, nadhani ndiye beki bora zaidi wa pembeni ambaye nimewahi kucheza naye," alisema Félix kuhusu klabu na mchezaji mwenzake wa kimataifa wa Ureno, Cancelo.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,154,8

MECHI KALI

BURNLEY VERSUS MANCHESTER UTD

1 | 4.03
X | 3.89
2 | 1.83

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# MOUNT, VARANE KUREJEA UNITED IKIIVAA BURNLEY

**MUNICH,** Ujerumani

MANCHESTER United ina matumaini Mason Mount na Raphaël Varane watakuwapo katika mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Burnley utakaochezwa leo, kwa mujibu wa ESPN.

Mount na Varane wamejiunga tena na mazoezi baada ya kukaa nje ya uwanja kutokana na majeraha, lakini hawakuwa fiti vya kutosha kusafiri hadi Ujerumani kwenye kichapo cha mabao 4-3 kutoka kwa Bayern Munich kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyofanyika Jumatano iliyopita.

Kuna matumaini wawili hao wanaweza kutajwa kwenye kikosi kitakachocheza kwenye dimba la Turf Moor.

Kikosi cha United kilisalia Munich usiku kucha na kufanya mazoezi katika akademi ya Bayern hapo juzi kabla ya kusafiri kwa ndege kurejea jijini Manchester.

Kocha Ten Hag hakuwa na wachezaji 12 waandamizi dhidi ya Bayern Munich na alilazimika kutaja makipa watatu kwenye benchi kwenye Uwanja wa Allianz Arena.

Kurejea kwa Mount na Varane dhidi ya Burnley kutamtia nguvu Mholanzi huyo lakini kuna hofu wachezaji wengine wawili waliojeruhiwa, Luke Shaw na Aaron Wan-Bissaka, wanaweza kukabiliwa na vipindi virefu vya nje ya uwanja.

Wan-Bissaka pia anaweza kuwa nje ya uwanja baada ya kupata jeraha la misuli ya paja dhidi ya Brighton.

United wamethibitisha kuwa beki huyo wa kulia atakosa kwa "wiki kadhaa" lakini inaweza kuwa zaidi ya miezi miwili.

# Levy afunguka ilipokosea Spurs

**LONDON,** England

MWENYEKITI wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy amesema ilikuwa "kosa" kuwaajiri Jose Mourinho na Antonio Conte kama makocha kwani klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu England "ilihitaji kurejea mizizi yake" na kocha mpya, Ange Postecoglou.

Machi, kocha wa zamani wa Juventus, Conte alikua kocha wa pili mwenye medali kadhaa za washindi kuondoka Kaskazini mwa London katika muda wa zaidi ya miaka mitatu.

Pia walimfukuza Mourinho miaka miwili iliyopita baada ya Mreno huyo kuletwa kuchukua nafasi ya Mauricio Pochettino.

Levy amekuwa akizongwa sana siku za nyuma, huku baadhi ya mashabiki wa Spurs wakimlaumu kutoshinda medali yoyote tangu mwaka 2008.

"Nataka kushinda kama kila mtu mwingine," alisema Levy kwenye kongamano la mashabiki.

"Kuchanganyikiwa kwa kutoshinda na shinikizo kutoka kwa baadhi na wachezaji na sehemu kubwa ya msingi ya mashabiki ambayo tunahitaji kushinda, tunahitaji kutumia fedha, tunahitaji kuwa na kocha mkubwa, jina kubwa. Na iliniathiri. "

Pochettino alitimuliwa mwaka 2019, miezi mitano tu baada ya kuiongoza Spurs kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Kocha huyo alikuwa na kibarua cha kuinoa Paris Saint-Germain kabla ya kuinoa Chelsea msimu huu wa joto.

"Nilikuwa nimepitia kipindi ambacho tungekaribia kushinda, na Mauricio tulipitia nyakati nzuri sana," alionGeza Levy.



61,566/-

# SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23.09.23 | 17:00 | Middlesbrough FC vs Southampton FC | 2.65 | 3.35 | 2.47 |
| 02. 23.09.23 | 17:00 | Dundee FC vs Kilmarnock FC | 2.50 | 3.20 | 2.70 |
| 03. 23.09.23 | 17:00 | Airdrieonians FC vs Raith Rovers FC | 2.43 | 3.20 | 2.55 |
| 04. 23.09.23 | 17:15 | CA Osasuna vs Sevilla FC | 2.50 | 3.20 | 2.70 |
| 05. 23.09.23 | 19:30 | Burgos CF vs Elche CF | 2.80 | 3.00 | 2.60 |
| 06. 23.09.23 | 19:30 | Werder Bremen vs 1. FC Cologne | 2.55 | 3.50 | 2.50 |
| 07. 23.09.23 | 19:45 | NEC Nijmegen vs FC Utrecht | 2.55 | 3.55 | 2.47 |
| 08. 23.09.23 | 20:00 | Casa Pia Lisbon vs Vitoria SC Guimaraes | 2.55 | 3.05 | 2.80 |
| 09. 23.09.23 | 22:00 | Stade Brest 29 vs Olympique Lyon | 2.55 | 3.50 | 2.50 |
| 10. 24.09.23 | 14:00 | FC Metz vs Strasbourg Alsace | 2.85 | 3.20 | 2.42 |
| 11. 24.09.23 | 15:30 | Ajax Amsterdam vs Feyenoord Rotterdam | 2.48 | 3.60 | 2.50 |
| 12. 24.09.23 | 17:00 | Cercle Brugge vs Union Saint-Gilloise | 2.65 | 3.40 | 2.45 |
| 13. 24.09.23 | 17:15 | Real Oviedo vs Real Valladolid | 2.75 | 2.85 | 2.70 |
| 14. 24.09.23 | 17:15 | Rayo Vallecano vs Villarreal CF | 2.55 | 3.40 | 2.55 |
| 15. 24.09.23 | 18:05 | Montpellier HSC vs Stade Rennes | 2.65 | 3.45 | 2.43 |
| 16. 24.09.23 | 21:45 | Torino FC vs AS Roma | 2.85 | 2.95 | 2.55 |
| 17. 24.09.23 | 22:00 | Atletico Madrid vs Real Madrid | 2.65 | 3.35 | 2.47 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 23/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1270 | Livingston vs Celtic | 8.76 | 5.57 | 1.26 |
| 15:00 | 1538 | Jahn Regensburg vs Sandhausen | 2.31 | 3.37 | 2.85 |
| 15:00 | 3396 | Girona vs Mallorca | 1.90 | 3.44 | 4.31 |
| 15:00 | 3799 | Brescia vs Venezia | 2.92 | 3.07 | 2.37 |
| 16:00 | 2297 | Green Eagles vs FC Muza | 2.40 | 2.74 | 3.04 |
| 16:00 | 2815 | Napsa Stars vs Zanaco | 2.10 | 2.77 | 3.68 |
| 16:00 | 2904 | Nkwazi vs Kansanshi Dynamos | 2.20 | 2.65 | 3.50 |
| 16:00 | 3304 | Troyes vs AJ Auxerre | 3.12 | 3.42 | 2.09 |
| 16:00 | 3721 | AC Milan vs Verona | 1.45 | 4.51 | 7.29 |
| 16:00 | 5748 | Forest Rangers vs Nkana FC | 2.47 | 2.57 | 3.17 |
| 16:30 | 2451 | Monchengladbach vs RB Leipzig | 4.94 | 4.63 | 1.58 |
| 16:30 | 3730 | Union Berlin vs Hoffenheim | 2.11 | 3.60 | 3.35 |
| 16:30 | 4388 | Borussia Dortmund vs VfL Wolfsburg | 1.79 | 4.03 | 4.13 |
| 16:30 | 4459 | Bayern Munchen vs VfL Bochum | 1.17 | 7.94 | 14.12 |
| 16:30 | 5603 | Augsburg vs Mainz | 2.62 | 3.59 | 2.57 |
| 17:00 | 1127 | Leicester vs Bristol City | 1.70 | 3.77 | 4.26 |
| 17:00 | 1588 | Rotherham vs Preston | 3.03 | 3.18 | 2.25 |
| 17:00 | 1604 | Dundee FC vs Kilmarnock | 2.44 | 3.23 | 2.73 |
| 17:00 | 1821 | Ipswich vs Blackburn | 1.65 | 3.91 | 4.36 |
| 17:00 | 2848 | Swansea vs Sheffield Wed | 1.92 | 3.42 | 3.62 |
| 17:00 | 2983 | Hibernian vs St Johnstone | 1.57 | 3.84 | 5.38 |
| 17:00 | 3199 | Luton Town vs Wolverhampton | 3.25 | 3.41 | 2.23 |
| 17:00 | 3332 | Carlisle vs Derby | 3.24 | 3.54 | 2.04 |
| 17:00 | 3842 | Crystal Palace vs Fulham | 1.96 | 3.49 | 3.95 |
| 17:00 | 4360 | Manchester City vs Nottingham | 1.21 | 6.65 | 13.50 |
| 17:00 | 4790 | Plymouth vs Norwich City | 3.13 | 3.62 | 2.02 |
| 17:00 | 4987 | West Bromwich vs Millwall | 2.00 | 3.32 | 3.47 |
| 17:00 | 5141 | Leeds vs Watford | 1.70 | 3.66 | 4.36 |
| 17:00 | 5401 | Middlesbrough vs Southampton | 2.41 | 3.38 | 2.64 |
| 17:15 | 1216 | Osasuna vs Sevilla FC | 2.52 | 3.20 | 2.94 |
| 17:15 | 1342 | Levante vs CD Eldense | 1.74 | 3.33 | 4.67 |
| 18:00 | 1861 | Nantes vs Lorient | 2.38 | 3.39 | 2.98 |
| 19:00 | 1376 | Sassuolo vs Juventus | 3.86 | 3.75 | 1.91 |
| 19:30 | 1948 | Burgos vs Elche | 3.07 | 3.02 | 2.31 |
| 19:30 | 2714 | Werder Bremen vs FC Koln | 2.55 | 3.60 | 2.63 |
| 19:30 | 3745 | Barcelona vs Celta Vigo | 1.37 | 5.09 | 8.10 |
| 19:30 | 5310 | Brentford vs Everton | 1.81 | 3.75 | 4.32 |
| 19:45 | 4512 | NEC Nijmegen vs Utrecht | 2.53 | 3.48 | 2.45 |
| 20:00 | 2208 | Concarneau vs St Etienne | 3.22 | 3.22 | 2.14 |
| 20:00 | 5188 | Basaksehir vs Galatasaray | 4.02 | 3.55 | 1.80 |
| 20:00 | 5646 | Angers vs Bastia | 2.02 | 3.23 | 3.52 |
| 21:00 | 1255 | Almere City vs PSV Eindhoven | 10.88 | 6.73 | 1.18 |
| 21:30 | 3506 | St. Pauli vs Schalke 04 | 1.81 | 3.71 | 3.86 |
| 21:45 | 3344 | Lazio vs Monza | 1.83 | 3.76 | 4.23 |
| 22:00 | 1280 | Brest vs Lyon | 2.55 | 3.60 | 2.63 |
| 22:00 | 2915 | Burnley vs Manchester Utd | 4.03 | 3.89 | 1.83 |
| 22:00 | 3440 | Almeria vs Valencia | 2.88 | 3.50 | 2.40 |
| 22:00 | 4197 | Alcorcon vs Huesca | 2.18 | 2.97 | 3.41 |
| 22:00 | 5843 | Heerenveen vs SBV Excelsior | 1.58 | 4.05 | 4.74 |
| 22:30 | 3347 | Porto vs Gil Vicente | 1.20 | 6.16 | 10.94 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# HATIMA YA TANZANIA KUANDAA FAINALI ZA AFCON 2027 J'TANO

**Na Adam Fungamwango**

HATIMA ya maombi ya Tanzania, Kenya na Uganda kuandaa fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027) itajulikana Jumatano katika mkutano utakaofanyika jijini Cairo, Misri kwa wajumbe kupiga kura.

Tanzania, Kenya na Uganda ziliwasilisha maombi ya pamoja na jana viongozi wake walikutana Dar es Salaam ili kupanga mikakati.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Said Yakubu alisema wameandaa mikakati imara ya kuhakikisha wanapata wenyeji ikiwamo kwenda kufanya kampeni za pamoja kwa njia za kidiplomasia.

"Makatibu wakuu wa wizara za michezo, kutoka nchini zetu tatu za Kenya, Uganda na Tanzania tulikutana, na tayari tumepokea barua kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), inayoeleza Septemba 27, mwaka huu ndio kura ya kuamua nani awe mwenyeji wa fainali hizo zitapigwa huko Cairo, kwa hiyo tuliona nchi zetu tulizoomba kwa pamoja tukutane tupange mikakati namna ya kupata ushindi, " Yakubu alisema.

Alisema baada ya hapo kulitarajiwa pia kuwa na kikao cha Mawaziri wa Michezo wa nchi hizo.

Alisema wanajipanga kwenda Misri kwa ajili ya kufanya kampeni ambazo zitakuwa na lengo la kuwashawishi wajumbe wawapigie kura kwa sababu kuna nchi nyingine zimeomba kuandaa fainali hizo.

"Kikubwa ambacho CAF wanataka kuangalia ni miundombinu ambapo kwa sisi hatuna shaka nalo, tunaendelea na maboresho ya Uwanja wa Benjamin Mkapa na pia tunatarajia kujenga viwanja vingine, tutatumia njia za kidiplomasia pamoja na kuwatumia viongozi wenye shawishi kama Rais wa TFF, Wallace Karia pamoja na Leodegar Tenga, ambaye aliwahi kuwa mjumbe wa CAF, natumai wiki ijayo tutakuwa na habari njema, tuombeane heri," alisema kiongozi huyo.

Kama maombi hayo yatafanikiwa itakuwa ni mara ya kwanza kwa Afrika Mashariki iliyoko chini ya Rais, Samia Suluhu Hassan, Yoweri Museveni (Uganda) na William Ruto wa Kenya kuweka historia.



Kocha wa makipa wa Ihefu SC, Manyika Peter (wa pili kushoto), akiwa na magolikipa wa timu hiyo yenye maskani yake Mbarali, Mbeya ambayo inashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara. **PICHA: MTANDAO**

# Baleke, Yao waweka rekodi Ligi Kuu Bara

INATOKA UK 24

na kuiongoza timu yake kupata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Tabora United.

Kwa upande wa Yao, yeye ameweka rekodi ya beki anayeongoza kwa 'assist' kwa sasa kwenye ligi hiyo huku akiwa na bao moja.


Beki huyo wa kulia mwenye nguvu na kasi anamzidi Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' ambaye pamoja na 'assist' mbili lakini hana bao.

Yao aliyesajiliwa msimu huu akitokea Asec Mimosas alifunga bao la kwanza akiwa na timu yake mpya Agosti 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam akiiwezesha Yanga kushinda mabao 5-0.

Siku hiyo hiyo alitoa 'assist' kwa Maxi Nzengeli aliyefunga bao la tano wakati Jumatano iliyopita kwenye uwanja huo alitoa pasi ya mwisho la bao pekee lililofungwa dakika za lala salama na kuipa ushindi Yanga iliyowakaribisha Namungo FC kutoka Ruangwa, Lindi.

Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea tena kuanzia Septemba 29, mwaka huu kwa JKT Tanzania kuivaa Kagera Sugar huku siku hiyo Coastal Union ikiwakaribisha Tabora United kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga.

Michezo
Jumamosi Septemba 23, 2023
Nipashe



Felix: Nilishindwa falsafa za Atletico UK. 21




Kiungo wa Simba, Clatous Chama (kulia), akiwania mpira dhidi ya kiungo mshambuliaji wa Coastal Union, Ibrahim Ajib katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi. Simba ilishinda mabao 3-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Baleke, Yao waweka rekodi Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

MSHAMBULIAJI wa Simba, Jean Baleke wa Simba na beki wa Yanga, Yao Kouasi ambaye ni raia wa Ivory Coast pamoja wameweka rekodi tofauti katika Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kumalizika kwa raundi ya tatu.

Baleke ameweka rekodi ya kufunga mabao katika mechi zote tatu mfululizo ambazo amecheza msimu huu.

Mkongomani huyo aliyesajiliwa msimu uliopita kipindi cha dirisha dogo alifunga bao moja katika mechi ya raundi ya kwanza Simba ikishinda mabao 4-2 dhidi ya Mtibwa Sugar, akafunga tena walipoivaa Dodoma Jiji, kabla ya kufanya hivyo kwenye mechi ya raundi ya tatu ambapo alifunga 'hat-trick' na kuipa timu yake ushindi wa mabao 3-0.

Hiyo inakuwa ni 'hat-trick' ya pili msimu huu, ya kwanza ikiwekwa na Feisal Salum wa Azam FC katika mechi ya ufunguzi iliyochezwa Agosti 16, mwaka huu

INAENDELEA UK 23

# Rasmi Inonga kuikosa Dynamos

## Jeraha lake litachukua siku 14 kupona, Ugando aomba radhi...

**Na Saada Akida**

BEKI tegemeo wa Simba, Hennock Inonga hatokuwa sehemu ya mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos kutoka Zambia kutokana na kushonwa nyuzi 13 kufuatia jeraha la mguu alilopata katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Coastal Union iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi.

Simba inatarajia kuikaribisha Power Dynamos katika mchezo wa marudiano utakaochezwa Oktoba Mosi, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Inonga alishindwa kuendelea na mchezo huo baada ya kuchanika juu kidogo ya kifundo cha mguu kutokana na kumizwa na winga wa Coastal Union, Hija Ugando dakika 20 ya mchezo huo.

Akizungumza na Nipashe, Daktari wa Simba, Edwin Kagabo alisema Inonga alipatiwa matibabu katika Hospitali ya Mkoa wa Temeke na kuruhusiwa kurudi nyumbani jana jioni.

"Inonga ameruhusiwa kutoka hospitali, na amepata jeraha pale pale alipoumia katika mechi iliyopita dhidi ya Tanzania Prisons, jambo zuri hajavunjika mfupa ni kidonda tu. Suala atakaa nje kwa muda gani inategemea na jinsi atakavyopona lakini haikuwa sehemu mbaya sana," alisema Kagabo.

Naye Daktari wa zamani wa timu hiyo na mwanachama wa Chama cha Madaktari wa Michezo Tanzania (TASMA), Cosmas Kapinga alieleza beki huyo hatakaa nje kwa muda mrefu kulingana na jeraha alilopata.

**Kapinga alisema kitaalamu mtu yoyote ambaye ameshonwa anatakiwa kukaa siku saba hala fu ndio anatolewa nyuzi, baada ya hapo kidonda kupona inachukuwa kati ya siku saba hadi 14.**

"Lakini kwa jeraha la Inonga kwa kuwa amepata shida kwenye mguu mmoja basi baada ya kuondolewa nyuzi anaweza kufanya mazoezi ya kujiweka sawa bila mguu uliopata shida kuusumbua. Baada ya siku 14 ndio atatakiwa kufanya mazoezi ya kusukumana na wenzake kwa sababu tayari kidonda kitakuwa kimepona," alisema Kapinga ambaye pia aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Tiba ya Shirikisho la Riadha Tanzania (RT).

Wakati huo huo, Ugando amemwomba radhi Inonga kwa kitendo kilichotokea akidai haikuwa dhamira yake kumuuzika nyota huyo na wala hakufikiria hali hiyo ingetokea.

Ugando alisema nia yake ilikuwa kuwahi mpira ili kufunga na hakufikiria beki huyo angewahi kufika katika eneo hilo.

"Nimwombe radhi Inonga, haikuwa kusudi baada ya tukio hilo niliishiwa neno lolote la kumwambia kwa kilichotokea, isitoshe pia sikuweza kuzungumza naye kutokana na sijui kifaransa hivyo kitendo changu cha kwenda kwenye gari ya wagonjwa kama kumpa pole.

Nilichokifanya hakikuwa kitendo kizuri, haikuwa dhamira yangu kwa sababu nilisababisha timu yangu pia kucheza pungufu kwa sababu ya kadi nyekundu, niwaombe radhi wadau wote wa soka, mashabiki wa Simba na Coastal Union, pamoja na viongozi wa timu zote mbili," alisema Ugando.

Katika hatua nyingine, baada ya timu yake kuvuna pointi tatu dhidi ya Coastal Union, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' ameweka wazi mechi hiyo ameitumia kwa ajili ya kuandaa 'silaha zake' kuelekea mchezo wa kimataifa.

Robertinho alisema katika mechi hiyo aliangalia mambo mawili makubwa ikiwamo kutoka mbinu mpya na kuwapa nafasi wachezaji wake wenye uzoefu kuendelea kutengeneza uelewano.

"Baada ya kucheza mechi yetu ya kwanza Zambia tulitoka sare ya mabao 2-2, tuliona jinsi walivyocheza na tuliporejea tukafanyia kazi changamoto zetu kwa kuwaongeza kitu ambacho leo (juzi) wamekifanya nilivyowaangiza.

Nimefurahishwa jinsi wachezaji walivyocheza, ninaimani tulikuwa na nafasi ya kupata mabao mengi zaidi ya matatu tuliyofunga, tumeutumia mchezo huu kujiandaa na mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Power Dynamos," alisema Robertinho.

Aliongeza timu yake ilikuwa na nafasi kubwa ya kupata idadi kubwa ya mabao kuanzia sita hadi saba, lakini kupata matatu si mbaya.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >